# KUCHUNGUZA DHAMIRA KATIKA RIWAYA YA KIU YA MOHAMED SULEIMAN MOHAMED

**JALGHM ABUAZOUM EMHEMMD ALI**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SHARTI PEKEE LA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2017**

## UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma tasinifu hii iitwayo ***Kuchunguza Dhamira katika Riwaya ya Kiu ya Mohamed Suleiman Mohamed,*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sharti pekee la kutunukiwa Digrii ya Uzamili (M.A) ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

____________________________

**Profesa, Emanuel Mbogo**

**(Msimamizi)**

Tarehe: ______________________

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

# TAMKO

Mimi, **JALGHM ABUAZOUM EMHEMMD ALI**, nathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

-------------------------------

Saini:

-------------------------------

Tarehe

## TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa Baba yangu mzazi Abuazoum Emhemmd Ali aliyeuza sehemu ya mali yake kwa ajili ya kunilipia ada ya shule.

## SHUKURANI

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufikia hatua hii ya kukamilisha utafiti wangu nilioufanya kwa miaka kadhaa. Yeye ndiye aliyenijaalia nguvu, uwezo wa fikra na utashi wa kufanya utafiti huu ambao leo hii nauhitimisha. Kwake yeye Allah nasema Alhamdulilahi Rabi laalamina.

Napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru sana msimamizi wangu Profesa Emmanuel Mbogo kwa kunifundisha na kuniongoza katika utafiti huu mpaka hatua hii tuliyofikia hivi sasa. Profesa hakuchoka katika kunielekeza na kunitia moyo hata pale nilipoonekana kukata tama. Profesa alinitaka niwe mvumilivu kwani siku moja nitamaliza shule na kutunukiwa shahada yangu.

Napenda pia kuishukuru familia yangu kwa kunijali na kunipenda. Watu wa familia yangu wamekuwa bega kwa began a mimi katika kipindi chote cha masomo yangu kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Kwa hakika sina cha kuwalipa zaidi ya kuwaombea dua kwa mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema na mwenye kurehemu. Mwenyezi Mungu awalipe malipo mema.

## IKISIRI

Mada ya utafiti huu ilikuwa ni Kuchunguza Dhamira katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman Mohamed. Mada hii iliundwa na lengo kuu na malengo mahususi. Lengo kuu la utafiti lilikuwa ni kuchunguza dhamira za kijamii katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman. Malengo mahususi ya utafiti yalikuwa ni kuchambua dhamira za kijamii zinazowasilishwa katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman na kuelezea mbinu za kifani zilizotumika katika kuwasilisha dhamira za kijamii katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman.

Data za msingi za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na ile upitiaji wa nyaraka ikitumika katika kukusanya data za upili. Data za utafiti zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Sosholojia.

Kimsingi, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa dhamira za kijamii zinazojitokeza katika riwaya ya *Kiu* ni usafi wa mazingira, mapenzi katika jamii, wizi na magendo, umaskini na ujasiriamali. Dhamira hizi zimewasilishwa katika riwaya ya *Kiu* kwa kutumia mbinu za kifani za matumizi ya barua, misemo, sitiari, tashihisi na taharuki.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** .......... **ii**

**HAKIMILIKI** .......... **iii**

**TAMKO** .......... **iv**

**TABARUKU** .......... **v**

**SHUKURANI** .......... **vi**

**IKISIRI** .......... **vii**

**YALIYOMO** .......... **viii**

**SURA YA KWANZA** .......... **1**

**1.0 UTANGULIZI NA USULI WA TATIZO LA UTAFITI** .......... **1**

1.1 Utangulizi .......... **1**

1.2 Usuli wa Utafiti .......... **2**

1.3 Tamko la Utafiti .......... **4**

1.4 Lengo Kuu la Utafiti .......... **4**

1.4.1 Malengo Mahususi .......... **5**

1.4.2 Maswali ya Utafiti .......... **5**

1.5 Umuhimu wa Utafiti .......... **5**

1.6 Mipaka ya Utafiti .......... **6**

1.7 Mpangilio wa Tasinifu .......... **6**

**SURA YA PILI** .......... **7**

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** .......... **7**

2.1 Utangulizi .......... **7**

2.2 Maana ya Riwaya .......... **7**

2.3 Historia na Chimbuko la Riwaya ya Kiswahili .................... 9
2.4 Uhakiki wa Riwaya ya Kiswahili .................... 10
2.5 Mkabala wa Kinadharia .................... 12
2.5.1 Nadharia ya Sosholojia .................... 12
2.6 Hitimisho .................... 14
**SURA YA TATU .................... 15**
**3.0 MBINU ZA UTAFITI .................... 15**
3.1 Utangulizi .................... 15
3.2 Eneo la Utafiti .................... 15
3.3 Sampuli na Usampulishaji .................... 15
3.4 Aina ya Data Zilizokusanywa .................... 16
3.5 Mbinu za Kukusanyia Data .................... 16
3.5.1 Uchambuzi wa Kimaudhui .................... 17
3.6 Uchambuzi wa Data .................... 17
3.6.1 Mkabala wa Kimaelezo .................... 17
3.7 Zana za Utafiti .................... 18
3.7.1 Kalamu na Karatasi .................... 18
3.7.2 Kompyuta .................... 18
3.7.3 Simu ya Mkononi .................... 18
3.8 Hitimisho .................... 19
**SURA YA NNE .................... 20**
**4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI .................... 20**
4.1 Utangulizi .................... 20

4.2 Dhamira katika Riwaya ya Kiu .......... **20**
4.2.1 Usafi wa Mazingira .......... **21**
4.2.2 Dhamira ya Mapenzi katika Kiu .......... **23**
4.2.3 Wizi na Magendo katika Jamii .......... **26**
4.2.4 Umaskini katika Jamii .......... **28**
4.2.5 Dhamira ya Ujasiriamali .......... **31**
4.3 Mbinu za Kifani katika Riwaya ya Kiu .......... **34**
4.3.1 Matumizi ya Mbinu ya Barua .......... **35**
4.3.2 Matumizi ya Misemo katika Kiu .......... **37**
4.3.3 Matumizi ya Sitiari katika Kiu .......... **39**
4.3.4 Matumizi ya Tashihisi .......... **40**
4.3.5 Matumizi ya Taharuki katika Kiu .......... **41**
4.4 Hitimisho .......... **44**
**SURA YA TANO .......... 45**
**5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO .......... 45**
5.1 Utangulizi .......... **45**
5.2 Muhtasari .......... **45**
5.1.1 Dhamira za Kijamii katika Riwaya ya Kiu .......... **45**
5.1.2 Mbinu za Kifani katika Riwaya ya Kiu .......... **47**
5.3 Hitimisho .......... **49**
5.4 Mapendekezo .......... **49**
**MAREJELEO .......... 50**

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI NA USULI WA TATIZO LA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu ulikusudiwa kufanywa kwa nia ya kuchunguza dhamira mbalimbali ambazo zinawasilishwa na Mohamed Suleiman katika riwaya yake ya *Kiu*. Kupita riwaya hii tumeainisha dhamira za kijamii pamoja na mbinu za kifani zilizotumiwa na mwandishi katika kuibua dhamira ndani ya riwaya hiyo.

*Kiu* ni riwaya ya Kiswahili inayoelezea hadithi ya Bahati, kijana mwanamke aliyelelewa akaleleka na sasa anakutana na Idi, mwanaume laghai. Iddi hakawii kumzonga Bahati kwa kamba ya mapenzi ya uwongo. Bahati akiwa kalowa mapenzi hajijui hajitambui, anang'amua kuwa Iddi kwa kweli hampendi yeye, bali nafsi yake mwenyewe, na yeye Bahati ni chombo tu cha kutimiza shauku zake za kilimwengu. Kama ndege aliyenaswa katika ulimbo, jitihada zake za kujipatia nusura zinamletea angamio.

Riwaya ya *Kiu* ilipata zawadi ya kwanza katika mashindano ya uandishi wa hadithi za kubuni katika lugha ya Kiswahili, ambayo yaliandaliwa mnamo mwaka 1970. Katika utafiti huu tumeshughulikia dhamira za kijamii zinazojitokeza katika riwaya hii na kisha tukaelezea mbinu za kifani ambazo zimetumika katika kuwasilishia dhamira za kijamii.

Kimsingi, tunapozungumza kuhusu dhamira za kijamii tuna maana ya dhamira ambazo zinaigusa jamii katika maisha yake ya kila siku katika Nyanja mbalimbali za

kimaendeleo. Masuala ya usafi wa mazingira, mapenzi, umaskini, ujasiriamali na wizi na magendo ni baadhi ya dhamira za kijamii kwa sababu zinaigusa jamii moja kwa moja.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Kazi ya fasihi ikiwemo riwaya huundwa na fani na maudhui ambavyo kwa pamoja ndivyo hutupatia kazi inayoitwa fasihi. Fani ni ule ufundi wa kisanaa unaotumiwa na mwandishi kuisana kazi yake ili wasomaji na wasikilizaji waweze kuifurahia (Njogu na Chimerah, 1999). Fani huundwa na vipengele kama vile wahusika, mtindo, mandhari, muundo na matumizi ya lugha. Vipengele hivi hutumiwa na waandishi kwa namna tofauti tofauti kulingana na ujuzi na welei wao. Kwa upande wa maudhui ni jumla ya mawazo makuu yanayoelezwa na mwandishi au msimulizi wa kazi ya fasihi na kutaka hadhira yake ipate (Simiyu, 2011). Maudhui hujumuisha vipengele vya dhamira, ujumbe, falsafa, migogoro na msimamo. Dhamira ni kipengele mama katika maudhui kwani ni katika dhamira ndipo wazo kuu la mwandishi linapopatikana.

Dhamira ni kipengele cha kimaudhui kinachopatikana katika kazi zote za fasihi riwaya ikiwemo. Watafiti kama vile Kezilahabi (1976) wamevutiwa na kufanya utafiti wa kuchunguza dhamira katika riwaya za Kiswahili hususani zile za Shaaban Robert. Mtaalamu huyu alifanya utafiti katika ngazi ya Shahada ya Uzamili akiwa na mada isemayo, “Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya.” Katika uchambuzi wake anabainisha kuwa riwaya za Kiswahili zimejaa utajiri mkubwa wa dhamira ambazo zinasawiri si jamii ya Watanzania peke yake bali duniani kote. Kwa mfano katika

riwaya za *Kusadikika*, *Kufikirika* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* za Shaaban Robert kunaelezwa masuala ya haki za binadamu ambayo yanagusa jamii mbalimbali za dunia. Ukweli huu unatoa hadhi kubwa kwa riwaya ya Kiswahili kwamba inao uwezo wa kushughulikia masuala ya jamii mbalimbali na si jamii moja ya Watanzania.

Riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman ni moja kati ya riwaya za Kiswahili yenye sifa ya kusawiri masuala yanayohusu jamii pana kama ilivyo kwa kazi za Shaaban Robert. Hili linathibitishwa na ushindi iliyopata riwaya hiyo katika miaka ya 1970 dhidi ya riwaya nyingine nyingi ambazo zilikuwa tayari zimeshaandikwa. Rashid (2015) alifanya utafiti wa kuchunguza namna majina yanavyolandana na vitendo pamoja na tabia za wahusika katika riwaya ya *Kiu* na *Nyota ya Rehema* za Mohamed Suleiman. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa uteuzi wa majina katika riwaya hizo mbili unalandana kwa kiasi kikubwa na vitendo ambavyo wahusika hao wanavifanya. Kwa mfano mhusika Idi anaonekana kuwa ni mtu mwenye mwenye tamaa na asiyeridhirika na kidogo alichonacho na kutamani utajiri zaidi. Hii inatokana na jina lenyewe katika taaluma ya Saikolojia Changanuzi tunaelezwa kuwa Idi ni nafsi ambayo huwa inamwamrisha mtu kufanya mambo maovu na kwa hiyo imesawiri vizuri hali ya maisha ya mhusika Idi katika riwaya ya *Kiu*.

Kimsingi, tunakubaliana na matokeo ya utafiti wa Rashid (2015) kuwa kwa kiasi kikubwa mwandishi amewajenga wahusika wake kulingana na majina yao. Hata hivyo, katika utafiti huu tumechunguza dhamira za kijamii zinazowasilishwa na mtunzi katika riwaya ya Kiu kwa lengo la kuendeleza mawazo ya Rashid (2015)

ambaye yeye hakuchunguza dhamira kama sehemu ya lengo lake kuu la utafiti.

## 1.3 Tamko la Utafiti

Riwaya ya Kiswahili ni moja kati ya tanzu nne za fasihi andishi ya Kiswahili huku nyingine zikiwa ni tamthiliya, ushairi na hadithi fupi (Wamitila, 2008). Utanzu wa riwaya ndio unaotumika kueleza mambo kwa kina na mapana zaidi kuliko tanzu nyingine za fasihi andishi. Kutokana na hali hii, riwaya huwasilisha dhamira za kisiasa, kijamii na kiutamaduni kwa jamii kwa kutumia visa na matukio yaelezwayo katika riwaya husika. Mohamed Suleiman ni mmoja kati ya watunzi wa riwaya za Kiswahili ambaye anatunga visa na matukio mbalimbali yatoayo dhamira zenye mashiko kwa jamii. Hata hivyo, mpaka kufikia hivi sasa hakuna utafiti wa kina ambao umefanywa kwa lengo la kuchunguza dhamira zinazojitokeza katika riwaya ya *Kiu*.

Wataalamu kadhaa kama vile Wamitila (2008; 2013) wamevutiwa sana na riwaya mpya za Kiswahili kama vile *Babu Alipofufuka* na *Dunia Yao* za Said Ahmed Mohamed na *Nagona* na *Mzingile* za Kezilahabi na kuzifanyia uchambuzi wa kina. Wakati hali ikiwa hivyo, kwa riwaya hizo mpya za Kiswahili, riwaya ya *Kiu* imekuwa ikitajwa tu na siyo kuchambuliwa kwa kina. Hivyo basi, utafiti huu ulifanywa kwa lengo la kuchunguza dhamira za kijamii pamoja na mbinu za kifani zilizotumika kuibulia dhamira katika riwaya ya *Kiu*.

## 1.4 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhamira za kijamii zinazojitokeza katika riwaya ya *Kiu*.

### 1.4.1 Malengo Mahususi

i) Kuchambua dhamira za kijamii zinazojitokeza katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman.

ii) Kuelezea mbinu za kifani zilizotumika katika kuwasilisha dhamira za kijamii katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman.

### 1.4.2 Maswali ya Utafiti

i) Ni dhamira zipi za kijamii zinazojitokeza katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman?

ii) Ni mbinu gani za kifani zilizotumika kuwasilishia dhamira katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa ni kumbukumbu ya kihistoria kuhusu riwaya ya *Kiu* kwa vizazi vijavyo kuelewa riwaya hii ilikuwa inahusu masuala gani. Kutokana na kufahamu historia hiyo watapata mambo ya kujifunza ambayo ni mazuri na yale ambayo ni mabaya watayaacha.

Wahakiki watauona utafiti huu kuwa ni rejeleo muhimu katika tahakiki zao watakazokuwa wanazifanya kwa nia mbalimbali. Walimu wa vyuo na sekondari watautumia utafiti huu katika kuimarisha ufundishaji wa fasihi andishi kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza mpaka cha sita na katika diploma na shahada mbalimbali. Watafiti wa ngazi mbalimbali watauona utafiti huu kuwa ni wa umuhimu mkubwa katika kuwawezesha kukamilisha malengo ya tafiti zao. Kutokana na utafiti huu watapata data za upili zitakazosaidia kukamilisha data za msingi za

utafiti wao. Pia watautumia utafiti huu kama kisima cha kujenga hoja za kufanya utafiti zaidi katika taaluma ya fasihi na husSee na husisani riwaya ya Kiswahili.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu utashughulikia riwaya moja ya *Kiu* tu. Riwaya hii imeandikwa na Mohamed Suleiman ambaye ameandika nyingine kadhaa. Katika utafiti huu tumeamua kushughulikia riwaya hii moja kwa sababu tuliamini kuwa itatupatia data tulizozihitaji ili kukamilisha utafiti wetu.

## 1.7 Mpangilio wa Tasinifu

Mpagilio wa tasinifu ni muundo wa utafiti mzima ulivyokuwa na ni sawa na kusema kwamba, ni ule muonekano na sura ya ripoti ya utafiti ulivyo. Tasinifu hii imeundwa kwa sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi; ambayo ina vipengele vya usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, malengo mahususi ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Sura ya pili ilihusu mapitio ya machapisho mbalimbali ambayo kwa namna moja au nyingine yanaelekeana na mada ya utafiti huu. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti ambazo zimetumika katika kukusanya na kuchambua data. Sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data na sura ya mwisho imehusika na muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti wa baadae.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Mapitio ya machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti ni muhimu mno katika kuwezesha utafiti wowote ule wa kitaaluma kukamilika. Katika sehemu hii tumefanya mapitio ya kazi tangulizi kadhaa ili kutoa uhalali wa kufanyika kwa utafiti wetu. Pia katika sura hii tumeeleza kuhusu nadharia iliyotumika katika kuchambua data za utafiti na kukazia ama kutoa msisitizo katika dhamira na mbinu za kifani zilizowasilishwa katika sura ya nne ya tasinifu hii.

## 2.2 Maana ya Riwaya

Maana ya riwaya imetolewa na wataalamu mbalimbali kwa kufanana katika baadhi ya vipengele na kutofautiana katika baadhi ya mambo yanayounda riwaya ya Kiswahili. Miongoni mwa wataalamu walioandika kuhusu dhana ya riwaya ni Nkwera (1978:109) pale anaposema: riwaya ni hadithi iliyo ndefu kuweza kutosha kufanya kitabu kimoja au zaidi. Ni hadithi ya kubuniwa iliyojengwa juu ya tukio la kihistoria na kuandikwa kwa mtindo wa ushairi uendao mfululizo kwa kinaganaga katika kuelezea maisha ya mtu au watu na hata taifa. Anaendelea kueleza kwamba, riwaya huwa ina mhusika mmoja au hata wawili.

Maana ya riwaya inayotolewa na Nkwera (ameshatajwa) inatufahamisha juu ya mambo muhimu kuhusu riwaya. Kwanza anatuambia kwamba riwaya ni hadithi ndefu jambo ambalo tunakubaliana nayo kwa asilimia mia moja. Riwaya ni hadithi

ndefu ambapo kutokana na urefu huo huifanya kuwa tofauti na ushairi na tamthilia au hadithi fupi. Urefu wa riwaya huifanya kueleza mambo kwa kina na marefu kiasi cha kumfanya msomaji kuelewa kisa, tukio au matukio mbalimbali yanayoelezwa katika riwaya husika.

Jambo lingine ambalo tumejifunza juu ya maana ya riwaya kutoka kwa Nkwera (1978) ni uwepo wa lugha au mtindo wa kishairi katika riwaya. Hapa tunafahamishwa kwamba, riwaya huweza kuandikwa kwa kutumia mitindo ya aina mbalimbali na sio ule wa insha ambao ndio uliozoeleka na watunzi wengi wa riwaya ya Kiswahili. Katika utafiti wetu tumeilewa dhana hii ya mtindo wa kishairi katika utunzi wa riwaya kuwa ni mwingiliano wa tanzu kama sehemu ya ubunifu katika utunzi wa riwaya. Katika utafiti wetu tumechungunza namna Mohamed Suleiman anavyotunga riwaya zake kwa kutumia mbinu mbalimbali za kifani kuibua dhamira.
Jambo ambalo tunakubaliana nalo kwa asilimia ndogo na Nkwera (ameshatajwa) ni kuhusu wahusika wa riwaya. Yeye anadai kwamba, riwaya inaweza kuwa na mhusika mmoja au hata wawili. Kwa hakika riwaya ni utungo ambao hueleza mambo kinaganaga kama alivyoeleza Nkwera (1978) mwenyewe katika maana aliyoitoa hapo juu. Kama hivyo ndivyo, ni wazi kwamba, riwaya yenye mhusika mmoja haiwezi kueleza mambo kinaganaga kama itakavyokuwa kwa riwaya yenye wahusika wengi. Mlacha na Madumulla (1991) wanasema kwamba, riwaya huwa inawahusika wengi ambapo kuna kuwa na mhusika mkuu na wahusika wadogo au wasaidizi ambao kazi yao kuu ni kumpamba mhusika mkuu aweze kukamilisha malengo ya mtunzi. Maelezo ya Mlacha na Madumulla (wameshatajwa) yanaonekena kuwa na mashiko ambayo ni ya kitaaluma zaidi kuhusu idadi ya

wahusika katika riwaya ya Kiswahili nasi tuliyachukua na kuyafanyia kazi katika utafiti wetu.

## 2.3 Historia na Chimbuko la Riwaya ya Kiswahili

Njogu na Chimera (1999) wanaeleza kwamba, historia ya riwaya ya Kiswahili inafungamana na historia ya maendeleo ya jamii za Afrika ya Mashariki. Hii ina maana kwamba, mtu anapotaka kueleza juu ya chimbuko la riwaya ya Kiswahili basi anapaswa kutazama maendeleo ya jamii ya Waswahili katika vipindi mbalimbali vya maendeleo yake kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Mulokozi (1996) anaeleza kuwa, chimbuko la riwaya ya Kiswahili lipo katika mambo makuu mawili ambayo ni; fani za kijadi za fasihi pamoja na mazingira ya kijamii. Maelezo haya yanaonesha kuoana na yale ya akina Njogu na Chimera (tumeshawataja) ambao nao wanasema kuwa, "chimbuko la riwaya ya Kiswahili ni ngano za kisimulizi." Mawazo haya tunakubaliana nayo kwa kiasi kikubwa kwa msingi kwamba, tanzu mbalimbali za fasihi ambazo tunazo katika maandishi riwaya ikiwemo zilianzia katika fasihi simulizi. Masimulizi ya ngano ndiyo yaliyochukuliwa na kutiwa katika maandishi na kuipata riwaya ya Kiswahili (Mulokozi, 1996).

Madumulla (2009) anafafanua zaidi juu ya chimbuko la riwaya ya Kiswahili kwa kukazia maarifa tuliyoyaona hapo juu kwa maelezo kwamba, riwaya ilitokana na nathari bunilizi kama vile hadithi, hekeya na ngano iliyosimuliwa kwa mdomo. Anaendelea kusema kuwa riwaya ilitokana na maandiko ya fani ya ushairi hususani tendi za Kiswahili katika hati za Kiarabu kwa sababu ndio maandishi yaliyotamba katika pwani ya Afrika ya Mashariki. Mawazo haya kwa hakika hatuna shaka nayo

kwa kuwa nayo yanaendelea kuonesha kwamba, riwaya ya Kiswahili inatokana na fasihi simulizi jambo linathibitisha kwamba, historia ya riwaya ya Kiswahili inaumana na historia ya Waswahili. Ngano zinazotajwa na Madumula (2009) ni hadithi ambazo watoto walisimuliwa na bibi au babu wakiwa wanaota moto usiku.

## 2.4 Uhakiki wa Riwaya ya Kiswahili

Riwaya ya Kiswahili imefanyiwa uhakiki na wataalamu kadhaa ingawa si kwa kiasi kikubwa. Mlacha na Madumulla (1991) wameandika kitabu chenye anuani isemayo *Riwaya ya Kiswahili*. Katika kitabu hiki kumeelezwa mambo mbalimbali yahusianayo na historia ya riwaya ya Kiswahili, maendeleo ya wahusika na mabadiliko katika dhamira za riwaya ya Kiswahili na kadhalika. Katika maelezo yao wanaeleza kuwa dhamira katika riwaya ya Kiswahili hubadilika kulingana na mazingira na mabadiliko ya maisha katika jamii. Mawazo haya yanatoa mchango muhimu katika kusukuma mbele utafiti huu kwa sababu katika utafiti wetu tulikuwa makini kuchunguza dhamira katika riwaya ya *Kiu* kwa kuzingatia muktadha wa kutungwa kwake.

Mulokozi (2013) amehakiki riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* katika muktadha wa Kihistoria. Anaeleza kwamba, riwaya hii ni mfano mzuri wa riwaya ya Kihistoria ambayo inaweza kuwa riwaya bora kabisa katika mkondo huo wa riwaya ya Kihistoria. Katika riwaya hii kumeelezwa mambo mengi ya Kihistoria ambayo ni urithi mkubwa kwa vizazi vijavyo ambavyo vitaisoma riwaya hii na kisha kufahamu mambo mbalimbali kuhusu nchi yao. Maelezo ya Mulokozi (1996) tunakubaliana nayo na kwamba yanasukuma mbele utafiti huu kwa kuwa hata riwaya ya *Kiu* ya

Mohamed Suleiman ni ya mkondo huo wa Kihistoria. Uhakiki wa Mulokozi umetupatia mbinu mbalimbali za kuihakiki na kuichambua riwaya ya aina hii na hivyo ilikuwa kazi rahisi kwetu kukamilisha utafiti huu.

Kyando (2013) anaeleza kuwa uteuzi wa majina ya wahusika katika kazi za riwaya hufanywa na mtunzi kwa namna ambayo jina la mhusika litafanana na kile ambacho anakifanya, tabia zake, maumbile yake, mahusiano yake na wenzake na kadhalika. Katika kufanya hivyo basi mtunzi anapata mhusika au wahusika sadfa. Katika maelezo yake anatoa mfano wa Mhusika "Mwinyi" katika *Kiu* kuwa ni mhusika ambaye anaendana kwa kila kitu na jina lenyewe. Maelezo haya yanatupatia mwangaza wa kufahamu kwamba, kupitia majina ya wahusika tunaweza kupata dhamira mbalimbali. Hivyo basi, katika utafiti wetu tulikuwa makini na matumizi ya majina ya wahusia ili tuweze kupata dhamira mbalimbali ambazo tulizihitaji kutoka katika riwaya ya *Kiu*.

Pia, Alli (2015) alifanya utafiti akichuguza namna majina yanavyolandana na tabia za wahusika katika riwaya za *Nyota ya Rehema* na *Kiu* zilizoandikwa na Mohamed Suleiman. Mtafiti anabainisha kuwa mwandishi amejitahidi kwa kiasi kikubwa katika kuhakisha kuwa matendo ya wahusika yanasadifiana na majina yao. Jambo hili lilituvutia sana na kutaka kuchunguza dhamira za kijamii katika riwaya husika ili hatimaye nasi tuone ni kwa vipi majina ya wahusika yanasaidia katika kujenga dhamira. Katika utafiti wetu tumechunguza dhamira za kijamii na kufanikiwa kuelezea mbinu za kisanaa zilizotumika katika kuwasilishia dhamira katika riwaya ya *Kiu*.

## 2.5 Mkabala wa Kinadharia

Katika sehemu hii tumewasilisha nadharia ya Sosholojia ambayo ndiyo iliyotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Nadharia hii imetumika katika kuchambua data zinazohusiana na dhamira za kijamii pamoja na mbinu za kifani zilizotumiwa na mwandishi katika kuibua dhamira.

### 2.5.1 Nadharia ya Sosholojia

Mwasisi mmojawapo wa nadharia ya Sosholojia ni Adam Smith ambaye alianzisha nadharia hii mwaka 1970 huko Marekani (Turner, 1999). Scott (1995) anasema kuwa nadharia ya Sosholojia imejikita zaidi katika kuangalia uhusiano wa mwanadamu na jamii yake. Wamtila (2002) anaeleza kwamba wahakiki wa Kisosholojia hushikilia kuwa kazi ya kifasihi imedhibitiwa na muundo wa kijamii, kiuchumi na kisiasa. Aidha, wahakiki hawa wanaamini kuwa jinsi wasomaji wanavyoipokea, kuitathmini na kuihukumu kazi fulani huathiriwa pia na mazingira ya wasomaji hao kiwakati na kimahali. Webster (2006) akifafanua juu ya nadharia ya Sosholojia anaeleza kuwa nadharia hii huikabili kazi ya fasihi kwa kuangalia jinsi inavyohusiana na mazingira ya kijamii. Nadharia hii huamini kuwa uhusiano kati ya kazi ya kifasihi na jamii ambayo kazi hiyo imeandikiwa ni muhimu sana. Anaendelea kufafanua kuwa sanaa haijengwi katika ombwe, ni kazi ya mwandishi katika mazingira na wakati maalumu akiwajibika kwa jamii inayomhusu ambayo ni sehemu yake muhimu. Mazingira ya jamii ndio huweza kubadili na kuathiri maudhui ya kazi ya fasihi.

Nadharia ya Sosholojia inahusika na kuchunguza mahusiano katika jamii ambayo yanatokana na matabaka yaliyopo katika jamii (Cross, 2011). Katika jamii kuna

matabaka ya walionacho na yale ya wasionacho na kwa namna moja au nyingine matabaka haya hutegemeana katika maisha yao ya kila siku. Tabaka la walionacho huwatumikisha watu wa tabaka la wasio nacho na wao kuendelea kupata zaidi na wale wa tabaka la wasionacho kuendelea kuwa maskini (Swingewood, 2000). Wakati mwingine ni vigumu kwa matabaka haya mawili kuwa na mahusiano ya kirafiki, yaani mtu wa tabaka la wasionacho akawa na urafiki na yule wa tabaka la walionacho (Skeggs, 1997). Kwa mfano, binti wa kutoka tabaka la wasionacho anaweza kumpenda kijana wa tabaka la walionacho lakini wa wazazi hasa wa kijana tajiri hukataa mtoto wao asioe binti wa kimaskini. Lakini ikiwa kijana wa kiume atokae katika familia tajiri ndiye aliyempenda binti wa kimaskini hufanya kila linalowezekana mpaka amuowe na mara nyingi hufanikiwa.

Nadharia hii ni muhimu katika utafiti huu kwa riwaya ya *Kiu* (1972) kwa sababu imezungumzia masuala ya kijamii kama vile uchumi, siasa, na utamaduni. Kimsingi, nadharia ya Sosholojia inazungumzia juu ya mahusiano ya wanajamii katika utendaji kazi wao na maisha yao ya kila siku. Kwa mfano, katika jamii huibuka migogoro baina ya mtu na mtu, mtu na jamii, jamii na jamii au jamii na serikali. Kazi ya Mwanasosholojia ni kuielewa jamii ambapo huangalia uhusiano wa jamii katika mienendo yao ya kila siku. Mienendo hiyo hulenga jambo linaloshughulikiwa na waandishi wa kazi za fasihi (Mbise 1996). Kwa kutumia nadharia hii tumeweza kutambua mahusiano ya kijamii katika riwaya ya *Kiu* na hatimaye kupata dhamira kijamii na kuweza kukamilisha utafiti huu. Pia, nadharia hii imetumika kuchambua vipengele vya mbinu za kisanaa vinavyopatikana katika riwaya ya *Kiu* na ambavyo

kimsingi ndivyo vilivyotumika katika kuwasilishia dhamira za kijamii katika riwaya hiyo.

## 2.6 Hitimisho

Katika sura hii tumepitia kazi tangulizi ambazo kwa namna moja au nyingine zinahusiana na mada ya utafiti huu. Tumepitia kazi tangulizi zinazohusiana na maana ya riwaya, historia ya riwaya ya Kiswahili, uhakiki wa riwaya ya Kiswahili na mkabala wa kinadharia. Kwa jumla, mapitio ya kazi tangulizi yanaonesha kuwa hakuna mtafiti hata mmoja ambaye amechunguza dhamira za kijamii katika riwaya ya Kiu ya Mohamed Suleiman ndipo nasi tukaona ipo haja ya kuchunguza dhamira hizo ili kuziba pengo hili la maarifa.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sehemu hii tumewasilisha mbinu za utafiti ambazo zilituongoza katika kufanikisha kupatikana kwa data za utafiti huu. Mbinu hizi zimewasilishwa baada ya kuzisoma kutoka kwa wataalamu mbalimbali wa mbinu za utafiti.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika jiji la Dar es Salaam hususani katika kukusanya data za msingi na fuatizi. Dar es Salaam imeteuliwa kwa sababu ndipo mahali ambapo maktaba zenye vitabu mbalimbali zinapopatikana ikilinganishwa na sehemu nyingine yoyote nchini Tanzania. Sababu ya pili ya kuteuliwa kwa Dar es Salaam ni kuwa ndipo mahali ambapo zinapatikana maktaba mbalimbali ambazo mtafiti alizitumia katika kusoma na kukusanya data za upili za utafiti huu.

## 3.3 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni wawakilishi au viwakilishi ambavyo huteuliwa kutoka katika kundi kubwa la jamii ili kuwa wawakilishi wa jamii nzima kama watafitiwa katika utafiti wowote ule wa kitaaluma na kitaalamu (Babbie, 1999). Utafiti huu ulikuwa na sampuli ya aina moja tu ambayo ni riwaya ya *Kiu*. Kwa mujibu wa utafiti huu sampuli hii ni muafaka katika kuwezesha kujibu maswali ya utafiti. Sampuli hii imeteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Sampuli lengwa, ni sampuli inayoteuliwa na mtafiti akiwa na imani kwamba, sampuli hiyo itampatia data anazohitaji na kwamba, akiteua sampuli tofauti na hiyo basi hatoweza kupata

data anazozihitaji (Creswell, 2009). Mtafiti aliamua kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa kwa sababu ni mbinu inayomwezesha mtafiti kuteua sampuli itakayompatia data za kutosha na za uhakika. Mtafiti hapotezi muda kwenda katika vyanzo ambavyo haviwezi kumpatia data anazozihitaji na hivyo kutumia muda wake vizuri.

### 3.4 Aina ya Data Zilizokusanywa

Utafiti huu ulikusanya data za msingi na upili. Data za msingi ni zile ambazo zitamlazimu mtafiti kuwa yeye ndiye wa kwanza kuzikusanya na kwamba, hakuna mtu yeyote ambaye alishawahi kuzikusanya kwa nia aliyonayo mtafiti wa sasa. Kothari (2008) anaziita data za aina hii kuwa ni ghafi yaani mpya kabisa ndio kwanza zinavumbuliwa. Kwa msingi huu, data za msingi za utafiti huu zilikusanya kutoka katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman.

Data za upili ni tofauti na zile za msingi kwa kuwa zenyewe zilikwishakusanywa na watafiti wengine na hivyo hazikusanywi kwa mara ya kwanza. Katika utafiti huu tulisoma makala, vitabu, majarida, magazeti na kadhalika ili kupata data za utafiti. Tulitenga muda wa kutosha kwa nia ya kusoma kazi tangulizi katika maktaba za Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Maktaba ya Taifa na ile ya Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar.

### 3.5 Mbinu za Kukusanyia Data

Data za msingi za utafiti huu zitakusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui kama inavyoelezwa hapa chini:

### 3.5.1 Uchambuzi wa Kimaudhui

Njia kuu iliyotumika katika kukusanya data za utafiti huu ni ile ya uchambuzi wa kikontenti ama “Content Analysis” kwa jina la Kiingereza. Kontenti ni maandishi au yaliyomo katika kazi husika. Kuhusiana na utafiti wetu, yaliyomo tuliyapata katika riwaya ya *Kiu*. Kwa kutumia mbinu hii tulisoma riwaya hii kwa kina kwa nia ya kupata data tulizozihitaji. Kila lengo mahususi la utafiti huu lilikuwa na mahali pake pa kuandikia data zilizopatikana kutoka katika riwaya hizo mbili. Babbie (1999) anaeleza kwamba, mbinu hii ni nyepesi sana katika kukusanya data kwa sababu mtafiti hatumii muda mwingi kuzunguka kuwatembelea watafitiwa. Kinachotakiwa ni yeye mtafiti kutafuta mahali maalumu ambapo ni patulivu kisha akakaa na kuanza kudondoa data anazozihitaji kutoka katika kazi ya fasihi aliyolenga kuichunguza.

## 3.6 Uchambuzi wa Data

Data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo kama inavyofafanuliwa hapa chini:

### 3.6.1 Mkabala wa Kimaelezo

Mbinu hii inaelezwa na Young (1984) kuwa ni mbinu ya uchambuzi wa data ambayo haihusishi mahesabu bali maelezo tu ndio hutolewa kuhusiana na data za utafiti zilizokusanywa. Baada ya kukusanya data, mtafiti alizipangilia vizuri kwa namna ambayo ilimwia rahisi kufanya uchambuzi. Mpangilio wa data hizo ulizingatia malengo mahususi ya utafiti huu. Baada ya kupangilia data hatua iliyofuata ilikuwa ni kuoanisha data ambazo zinafafana na kutenganisha zile zinazotofautiana. Nia ya kufanya hivi ni ili kurahisisha uchambuzi wa data ili ufanyika kwa muda mfupi.

Hivyo, data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo ambapo maelezo ya kina yalitolewa kwa namna ambayo imesaidia kukamilisha malengo mahususi ya utafiti huu.

### 3.7 Zana za Utafiti

Utafiti huu ulitumia zana mbalimbali katika kukusanya data pamoja na kuzifanyia uchambuzi. Zana hizo ni pamoja na:

#### 3.7.1 Kalamu na Karatasi

Kalamu na karatasi ni zana muhimu katika kurahisisha zoezi la ukusanyaji na uchambuzi wa data. Kalamu ilitumika katika kudondoa na kunukuu data kutoka katika riwaya husika pamoja na data kutoka katika kazi tangulizi tulizosoma maktabani. Karatasi ilitumika kuhifadhia data za utafiti zilizokusanywa ili zifanyiwe uchambuzi.

#### 3.7.2 Kompyuta

Komputa ilitumika katika kuchapisha na kutoleshea rasimu mbalimbali za utafiti huu mpaka kukamilika kwake. Pia, tulitumia kifaa hiki katika kupakuwa data kutoka katika wavuti na tovuti kwa nia ya kuimarisha utafiti wetu.

#### 3.7.3 Simu ya Mkononi

Kifaa hiki kilitumika katika kufanya mawasiliano na watu mbalimbali ambao walihusika na utafiti wetu kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, katika kuweka miadi ya kukutana na msimamizi wangu wa utafiti nilitumia simu ya mkononi ili

kufahamu kama yupo ofisini au hayupo ili nisipoteze muda mrefu kwenda wakati hayupo.

### 3.8 Hitimisho

Sura hii imewsilisha mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data. Data za utafiti zimekusanya kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui ambapo riwaya ya Kiu ilisomwa kwa makini ili kuweza kupata data za msingi. Mbinu ya mkabala wa kimaelezo ndiyo iliyoteuliwa kutumika katika kuchambua data za utafiti ambapo maelezo ya kina yalitolewa kwa kila data iliyowasilishwa.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti hufanywa pale tu data za utafiti zinapokuwa tayari zimeshakusanywa na kupangiliwa vizuri kwa namna ambayo inasaidia kujibu maswali ya utafiti. Hii ni hatua muhimu katika utafiti kwa sababu ndiyo inayokusudiwa ibainishe matokeo ya utafiti na kutatua tatizo la utafiti. Hivyo, uchambuzi wa data za utafiti huu umefanywa kwa kurejelea malengo mahususi ya utafiti huu ambayo yalikuwa ni kuchambua dhamira zinazojitokeza katika riwaya ya *Kiu* ya mwandishi Mohamed Suleiman na kubainisha mbinu za kifani zilizotumika katika kujenga dhamira katika riwaya ya *Kiu* iliyoandikwa na Mohamed Suleiman. Katika uchambuzi wa data za utafiti huu tumeanza na data zinazohusiana na lengo mahususi la kwanza na kisha lengo mahususi la pili.

## 4.2 Dhamira katika Riwaya ya Kiu

Dhamira ni mojawapo kati ya vipengele vinavyounda maudhui katika kazi ya fasihi huku vipengele vingine vikiwa ni migogoro, ujumbe, falsafa, msimamo na mtazamo wa mwandishi (Njogu na Chimerah, 1999). Wamitila (2008) anaeleza kuwa dhamira ni yale mawazo makuu ambayo yamemsukuma mwandishi wa kazi ya fasihi kuyaandika na yanajibainisha vizuri katika kazi husika. Kezilahabi (2003) anaiona dhamira kuwa ni lengo kuu la mtunzi wa kazi ya fasihi ambalo analilenga liifikie hadhira aliyoiteua. Mtaalamu huyu anakwenda mbali zaidi na kueleza kuwa si kila mtu anaweza kuwa ni hadhira ya kazi fulani ya fasihi kwa sababu kila mwandishi

huandika kazi yake akiwa na lengo kuu ambalo anataka hadhira yake ilipate. Hilo lengo kuu ndilo ambalo linafahamika kama dhamira ya mwandishi.

Dhamira ya mwandishi kwa kawaida hugawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo. Dhamira kuu ni ile ambayo inakuzwa na kujitokeza katika kazi nzima ya fasihi na dhamira ndogondogo ni zile ambazo zipo kwa ajili ya kuikamilisha dhamira kuu. Watunzi wa kazi za riwaya kama vile Mohamed Suleiman ambaye ni mwandishi wa riwaya ya Kiu ameitunga riwaya yake ikisheheni utajiri mkubwa wa riwaya zenye mafunzo kwa jamii ya Watanzania na hata wasiokuwa Watanzania. Dhamira zilizojitokeza katika riwaya ya *Kiu* ni nyingi lakini katika utafiti huu tumeteua dhamira za usafi wa mazingira, mapenzi katika jamii, nafasi ya mwanamke katika jamii, wizi na magendo, umasikini, malezi ya mama, ujasiriamali na usasa wa fikra.

### 4.2.1 Usafi wa Mazingira

Mazingira ni jumla ya vitu na mambo yote ambayo yanamzunguka mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. Vitu na mambo hayo yanayomzunguka mwanadamu ni pamoja milima, mabonde, mito, bahari, miti, majani, wanyama pori, makazi, taasisi za elimu, afya, utawala wa kiserikali, dini, mila na desturi na maziwa kutaja kwa uchache (Skeggs, 1997). Vitu hivi vyote vinayo nafasi kubwa katika kumfanya mwanadamu aweze kuishi maisha ya amani na utulivu na yenye afya tela. Pamoja na ukweli kuwa mazingira ni vitu ambavyo vimemzunguka mwanadamu lakini pia naye mwanadamu ni sehemu ya mazingira hayo. Mwanadamu anao uwezo wa kuyastawisha au kuyaangamiza mazingira kwa njia mbalimbali. Pale

anapoyaimarisha mazingira ndipo mazingira hayo yanapokuwa na manufaa kwa mwanadamu huyo wa sasa na kizazi kijacho. Kwa mfano, ikiwa mwanadamu atadumisha misitu kwa kupanda miti mingi na kila mara anapokata mti anapanda miti, mvua za kutosha zitanyesha na tatizo na upungufu au ukosefu wa chakula litakoma. Kinyume chake, ikiwa mwanadamu kazi yake ni kukata miti bila ya kupanda miti mingine kiwango cha mvua kitakuwa duni na jamii itakabiliwa na uhaba wa chakula (Turner, 1999).

Usafi wa mazingira ni jambo muhimu ambalo linaifanya jamii kuwa na aidha na afya njema au mbaya kama mazingira hayakusafishwa ipasavyo. Hivi leo katika mikoa mingi ya Tanzania kumeripotiwa kuwa na wagonjwa wengi wa ugonjwa wa kipindupindu ambao ni ugonjwa wa mlipuko utakanao na uchafu wa mazingira. Katika riwaya ya *Kiu* kunabainishwa kuwa uchavu wa mazingira ni tatizo ambalo linaikabili jamii ya Watanzania. Hebu tuone kifungu kifuatacho kutoka katika riwaya ya *Kiu*:

> *Idi alitangulia na Mwinyi akajikongoja na kumfuata. Njia zilikuwa mbaya, za kukatakata, za panda-shuka, vichochoro vichafu vyenye mawe yaliyootea. Mwinyi hakujali, maana hamu yake ilimpa nguvu. Alikaza miguu njiani kwa msaada wa mkongojo wake wa mpingo, moyoni akiwaza na kuota (uk.03).*

Katika kifungu hicho hapo juu inaonekana kuwa katika jamii kuna tatizo la uchafu wa mazingira kutokana na watu kutokuwa na tabia ya kufanya usafi katika maeneno yao. Vichochoro, mifereji ya maji taka na taka zisipozolewa kwa wakati na kupelekwa mbali na makzi ya watu husababisha mlipiko wa magonjwa kama kipindupindu, kichocho, kuharisha na homa za matumbo. Watu wengi wa Tanzania wamejenga fikra vichwani mwao kuwa mwenye jukumu la kufanya usafi katika

maeneo yao ni serikali na kusahau kwamba wao ndio wadau wa kwanza wa usafi katika makazi yao na mahala pa kazi. Sherehe juu ya nadharia ya Sosholojia zinazotolewa na wataalamu zinaeleza kuwa ni kawaida kwa wanadamu kukimbia wajibu na majukumu yao na kumwachia mtu mwingine (Swingewood, 2000). Haiingii akilini kwamba mtu binafsi ndiye anayetumia kila kitu katika nyumba yake na kuzalisha uchafu na taka halafu serikali ndio ifanye usafi. Mtu wa kwanza kuwajibika kuwajibika na usafi wa mazingira ni yule mtu anayeishi katika mazingira husika.

Serikali ya awamu ya tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeamua kuchukua jitihada za makusudi katika kuhakikisha kuwa wananchi wanakuwa na utamaduni wa kufanya usafi katika mazingira yao. Kwa mara ya kwanza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifuta sherehe za Uhuru za mwaka 2015 ambazo zilitakiwa kufanyika tarehe 9 mwezi 12 na kuagiza sikukuu hiyo isherehekewe kwa watu wote kufanya usafi. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliongoza shughuli za kufanya usafi kwa kushirikiana na wananchi wanaofanya biashara katika soko la samaki la feri jijini Dar es Salaam. Hivyo, ikiwa kila mwananchi atajitahidi kufanya usafi katika eneo lake mazingira yatakuwa safi na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu yatatoweka kabisa.

### 4.2.2 Dhamira ya Mapenzi katika Kiu

Mapenzi ni moja kati ya dhamira mardudi inayojitokeza katika kazi za fasihi andishi na simulizi kwa usawiri wa namna tofauti tofauti. Wapo watunzi wanaosawiri

dhamira ya mapenzi ya kingono, mapenzi ya mtu na mtu, mapenzi ya mtu na nchi yake, mapenzi ya mtu na familia yake, mapenzi ya mtu na ndugu zake, mapenzi ya mtu na mali kutaja kwa uchache. Wasanii wa nyimbo za Bongo Fleva kwa mfano, wanaeleza kuwa katika maisha ya siku hizi mapenzi yamekuwa ni kama bidhaa na mtu hasa mwanamke huwa na mapenzi na mtu mwenye mali na asiye na mali humweka kando (Omary, 2009). Mapenzi ya aina hii yanajitokeza katika riwaya ya Kiu ambapo tunaona mawazo ya Iddi yakithibitisha kuwa wapo wanawake ambao huwapenda wanaume kutokana na uwezo wa mali wa mwanaume. Tazama kifungu hiki:

> Ati watu husema mapenzi hayakutani, *mbona* yako wewe na Bahati yamekutana? Wacha masihara Iddi, Mwinyi alimkaripia. "Unafikiri mtoto kama yule, anaweza kumpenda mzee kama mimi?" "Yawezekana," Iddi alimjibu. "*Unajua* wanawake hupenda nini?… Wao ni viumbe wasiojimudu, hutafuta pa kuegemea, wanahusudu uwezo tu. Jiangalie wewe ulivyo: tajiri unayesifika, tena hizo mvi zako si alama ya ukosefu hata kidogo, ni alama ya busara tupu, huoni? (uk. 05)."

Kifungu hicho hapo juu kinabainisha kuwa katika jamii kuna mapenzi ya mali na si mapenzi ya dhati. Mzee Mwinyi haamini kuwa msichana mdogo ambaye ni mzuri kwa kila aina ya sifa anaweza kumpenda mzee kama yeye. Lakini Iddi anamtoa wasiwasi kuwa mbona hilo linawezekana na halina mashaka. Hii ni kutokana na wanawake walio wengi kumpenda mtu kutokana na uwezo wake wa kifedha na kukosekana kwa mapenzi ya dhati baina ya wawili hao. Sababu kubwa inayowafanya wasichana wadogo kuwa na mapenzi ya kingono na watu wazima ambao baadhi yao wanaweza kuwa sawasawa na wazazi wao kiumri ni kutokana na umasikini (Skidmore, 1979). Mtoto anayezaliwa katika hali ya umasikini na anataka kuishi katika maisha mazuri anajikuta ameingia katika mapenzi na mtu mzima aliye sawa

na baba yake au hata zaidi. Wanasosholojia wanakiri kuwa kila mtu katika jamii hupenda kuishi katika maisha mazuri na hata kwa kufanya mambo yasiyokubalika katika jamii basi atafanya ili ahakikishe kuwa anafanikiwa. Watu masikini katika jamii huchekwa na kudharauliwa na katika hali ya kawaida hakuna mtu anayekubali kudharauliwa kutokana na umasikini alionao (Diegner, 2011).

Kumbe basi, mapenzi baina ya mzee na kijana ni kitu ambacho kinawezekana kabisa na hakuna mwenye uwezo wa kupinga kitu hiki. Vile vile, ni jambo lililozoeleka kuona kijana wa kike akiwa na mahusiano ya kimapenzi na mzee wa kiume kuliko kijana wa kiume kuwa na mahusiano kama hayo na mzee wa kike. Hata hivyo, hii haina maana kuwa hakuna vijana wa kiume wanaokuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanawake ambao ni wazee (Held na MacGrew, 2007). Mapenzi hayachagui kijana au mzee bali mtu anaweza kumpenda yeyote yule. Mtunzi wa riwaya ya *Kiu* anabainisha kuwa:

> Asemaye mapenzi ni ya kijana tu, Mwinyi angemkana kwa kinywa kipana. Miaka sitini na miwili aliyoishi, hisia zake zilikuwa zikimtembea katika malimwengu huru. Pale alipofika, miezi sita iliyopita, kiasi angekanusha kuwa mapenzi ni neno la lugha tu si sehemu ya uhai wa mwanadamu, hayapo duniani; yakiwapo basi yanamuogopa. Leo, akilalama kwa sauti yenye kitetemeshi jinsi mapenzi yanavyomtenda. Akijua sasa kuwa mapenzi ni nguvu zilizozidi nguvu; ni machozi; ni mhanga; ni ukiwa; ni upweke; ni unyonge na maonevu; ni kutaka ukakosa. Katika miezi sita ile alikwishaziona shida zake, lakini raha zake bado (uk. 05).

Kifungu hiki kinathibitisha kuwa mapenzi haya umri kwani mzee anaweza kumpenda kijana na kinyume chake pia. Hii inafanana na kinachosawiriwa katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* ambapo mhusika anayeitwa Bwana Raza mwenye umri wa miaka 52 alipenda binti mgogo aliyekuwa ndio kwanza kavunja ungo akiwa na umri

wa miaka 15 (Abdallah, 2014). Kinachoonekana katika kifungu hiki cha maneno ni kuwa mara nyingi mzee wa kiume huwa na mapenzi ya dhati kwa binti mdogo lakini binti akawa hakumpenda mzee huyo kwa dhati bali kutokana na fedha zake. Mapenzi ya namna hii huwa hadumu kwani utajiri wa mali na fedha ni vitu ambavyo leo vipo na kesho havipo kwa hiyo huyo mwanaume mzee anapokosa fedha hukimbiwa na mpenzi wake ambaye ni binti mdogo. Kutokana na hali hiyo baadhi ya wazee hupata matatizo ya presha, kisukari na kiharusi kutokana na mawazo na simanzi aliyoachiwa kutokana na kutorokwa na binti huyo (Scott, 1995).

### 4.2.3 Wizi na Magendo katika Jamii

Wizi na magendo ni njia za kujipatia mali na fedha kutokana na biashara au kazi ambazo si halali kisheria. Kwa mfano, mtu au kikundi cha watu kinavamia nyumba ya mtu na kupora vitu vya thamani kama fedha, simu, kompyuta, televisheni na redio na kisha kujipatia utajiri kutokana na wizi huo. Pia, baadhi ya watu hufanya vitendo vya wizi kwa kutumia silaha na kuiba fedha katika mabenki na maduka ya wafanyabiashara na kujipatia utajiri. Baadhi ya watu hufanya wizi wa kughushi na wengine kuibia serikali au taasisi wanapofanyia kazi. Wizi wa aina hii huhusishwa pia na rushwa na ufisadi (Khamis, 2007). Magendo huhusishwa na kufanyabiashara bila ya kufuata kanuni na sheria kama vile kuwa na leseni na kulipa kodi. Kutokana na ukwepaji wa kodi mfanya magendo hupata utajiri mkubwa.

Katika nchi ya Tanzania kumekuwa na tatizo kubwa la wizi na magendo kiasi cha kuikosesha serikali mapato mengi ambayo yangesaidia katika kutoa huduma za jamii kama elimu, afya, maji, barabara na umeme (Diegner, 2011). Baadhi ya watumishi

wa serikali wamekuwa wakipata utajiri kutokana na kujilimbikizia mali kutokana na vitendo vya rushwa na ufisadi. Mohamed Suleiman katika riwaya yake ya *Kiu* anasema:

> "Sikia Bahati mpenzi," Iddi aliendelea kumsihi, "wale waliotajirika, wote ni wezi. Mwizi si yule mtu anayevunja nyumba tu. Tuseme huyu mzee utajiri wote ameupata wapi?" Alimuuliza na halafu akajibu mwenyewe, ameurithi … Nani asiyejua kuwa baba yake alikuwa mwizi wa magendo? Na yule mwenzake, nani yule … naam. Tumbe. Mzee Tumbe ametajirika kwa kukopesha riba! Hebu nitajie karani au dereva aliyetajirika kwa kazi yake peke yake (uk.15)?"

Kifungu hiki cha maneno kinaonesha kuwa wapo wanajamii wengi ambao wanapata utajiri kutokana na wizi wa magendo. Hali hii imezoeleka na kuonekana kuwa ni kitu cha kawaida mtu kupata utajiri kwa kutumia njia zisizokubalika ndio maana Iddi anamsihi Bahati kumkubali Mzee Mwinyi awe mpenzi wake ili waweze kumwibia utajiri wake na wao waondokane na umasikini. Haya ni maneno yanayotoa ushahidi kuwa ile dhana ya kuwa utajiri hupatikana kutokana na watu kufanya kazi imetoweka na sasa watu wanatafuta utajiri kwa kutumia wizi na magendo. Hali hii inawafanya wanajamii kubweteka na kuamini kuwa ni kweli wizi na magendo ndio njia muafaka ya kuweza kupata utajiri.

Mtaalamu wa masuala ya kisosholojia Ritzer (2008) anaeleza kuwa mwanadamu ni mtu mwenye tamaa ya mali na kila mara hutaka kuwa ndiye mtu mwenye mali kulio wanajamii wote. Ili kuweza kutimiza tamaa yake hutafuta njia rahisi na ya mkato ambayo itaweza kumpatia utajiri wa haraka haraka. Ni kutokana na hali hii ndio maana baadhi ya wanadamu hujiingiza katika vitendo vya wizi, ubadhirifu wa mali za umma, rushwa na ufisadi ili wapate mali za harakaharaka. Tabia hii inapaswa

kupigwa vita kwa nguvu zote kwani ikiachiwa iendelee italeta madhara makubwa kwa jamii. Kwa mfano, katika nchi ya Tanzania iliripotiwa katika magazeti kuwa mtumishi mmoja wa mamlaka ya mapato amejilimbikizia mali kiasi cha kumiliki nyumba zaidi ya 100 na zote zikiwa katika jiji la Dar es Salaam. Huu ni ufisadi mkubwa wenye kuonesha namna mwanadamu alivyo mbinafsi mwenye kutaka kujilimbikizia mali yeye binafsi huku wanadamu wenzake katika lindi la umasikini. Haingii akilini mtumishi wa serikali kuwa na utajiri mkubwa kiasi hicho hali ya kuwa kuna Watanzania wengine wanalala nje kwa kukosa hata kibanda cha kuwasitiri. Sheria kali zinatakiwa kuchukuliwa dhidi ya watumishi wa aina hii ili iwe funzo kwa wengine (Cross, 2011).

### 4.2.4 Umaskini katika Jamii

Umaskini ni dhamira kongwe katika ulimwengu wa fasihi ikijolkeza katika kazi za fasihi simulizi na andishi (Mlacha, 1987). Umaskini ni jambo ambalo limekuwa likiibali jamii ya Watanzania kwa miaka mingi na serikali imefanya jitihada kubwa ya kuhakikisha kuwa jamii inaondokana na umaskini. Umaskini ni hali ya mtu, jamii au taifa kutokuwa na uwezo wa kumudu gharama za mahitaji ya maisha yake ya kila siku ikiwemo chakula, malazi, mavazi, huduma za afya na elimu. Umaskini wa aina hii umekuwa ukiisumbua jamii tangu kupatikana kwa uhuru wa Tanzania katika mwaka wa 1961 (Diegner, 2011). Serikali ya Tanzania ilibua sera na kauli mbiu mbalimbali zenye kuhimiza wananchi kufanya kazi kwa bidii ili kukabiliana na umaskini. Baadhi ya kauli mbiu hizo ni “kilimo ni uti wa mgongo wa taifa,” “kilimo cha kufa na kupona,” na “siasa ni kilimo.” Kauli mbiu hizi zilitolewa na viongozi wa serikali ya awamu ya kwanza wakiongozwa na baba wa taifa mwalimu Julius

Kambarage Nyerere (Nyerere, 1977). Lengo hasa la kauli mbiu hizo lilikuwa ni kuihamasisha jamii ifanye kazi kwa bidii ili iweze kuwa na maisha bora.

Serikali zilizofuata nazo zilijitahidi kwa kiasi kikubwa kuhakisha kuwa umaskini unaondoka kwa kuanzisha mikakati na sera mbalimbali. Kwa mfano, serikali ya awamu ya tatu chini ya utawala wa mheshimiwa rais Benjamin William Mkapa ilikuja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania. Mkakati huu ulilenga kukuza sekta ya kilimo, mifugo, elimu, afya, huduma za maji safi na salama, umeme vijijini na viwanda. Mkakati huu ulisaidia sana katika kukuza sekta ya elimu ambapo mpaka hivi sasa karibu kata zote Tanzania zina shule za sekondari. Hata hivyo, sekondari hizo bado zinakabiliwa na upungufu wa walimu, vitabu, madawati, nyumba za walimu, mabweni, miundo mbinu ya maji, umeme na maabara. Jambo ambalo serikali inaendelea kukabiliana nalo ni kuhakikisha kuwa shule zote zinapata mahitaji yote ya muhimu ili zitowe elimu bora kwa wananchi.

Suala la umaskini wa kipato cha wananchi kuweza kuwa na uhakika wa kupata mahitaji ya muhimu kama vile chakula bado ni kidogo sana kwa Watanzania walio wengi (Kyando, 2013). Hili linasawiriwa katika riwaya ya *Kiu* kama mwandishi anavyosema:

> Bahati alivuta mbuzi ya kukunia nazi akaikalia kando ya sahani za chakula. Huku anamtazama mama, alifungua kinywa kwa mafunda ya chai, akaokota pande la mhogo na kujitafunia.
> Alikula kama mwenye kulazimishwa na kuvitazama vile vyakula mbele yake kwa jicho la dharau. Alichukua kipande cha mkate akakichovya katika chai, akakipuliza kidogo na kukishindilia kinywani. Alikuwa amechoshwa na vyakula vya aina moja kila siku (uk. 24).

Kifundu cha maneno hapo juu kinathibitisha kuwa umaskini bado ni tatizo kubwa katika jamii kiasi kwamba wanajamii hawana uwezo wa kula aina ya vyakula ambavyo wanavipenda. Hali ya mtu kula chakula cha aina ileile tu katika maisha yake ya kila siku kinaashiria kuwa mtu huyo anakabiliwa na umaskini (Khamis, 2007). Kula chakula cha aina moja tu kila siku ni jambo linalochosha na kumfanya mlaji kutokuwa na hamu ya kula. Katika kifungu cha maneno hapo juu inaelezwa kuwa mhusika Bahati hakupenda kula chakula hicho hicho kila siku lakini alilazimika kutokana na hali ya umskini iliyoikabili familia yake. “Alikula kama mwenye kulazimishwa na kuvitazama vile vyakula mbele yake kwa jicho la dharau,” ni kauli inayoashiria kwamba Bahati alichoshwa na vyakula vya aina moja kila siku. Wananadharia ya Sosholojia wakiongozwa na Webster (2006) wanadai kuwa chakula ni kitu cha kwanza kabla ya mwanadamu kufikiria kufanya jambo lingine katika maisha. Hii ina maana kuwa kama mtu akiwa hajala chakula akashiba au anakula kwa kujilazimisha tu ni wazi kuwa hawezi kuwa na fikra za kiubunifu wa kimaendeleo. Hii inasababishwa na hali yake ambapo kila mara atakuwa akifikiria kuhusu chakula na hata fanya mambo mengine ya msingi.

Kula chakula cha aina moja kila siku ni dalili ya umaskini na kwamba kama Bahati na familia yake wangekuwa na uwezo wa kifedha wangeweza kununua vyakula chungu tele vinavyopatikana katika masoko. Vyakula hivyo ni mchele, ndizi, viazi, sembe, halua, tende na vinyaji aina kwa aina. Lakini kutokana na umaskini, Bahati na familia yake waliishia kula mhogo, mkate na chai kila siku. Hata hivyo, tunakiri kuwa umaskini wa aina hii ni bora zaidi kuliko umaskini wa kukosa kabisa (Mlacha, 1991). Wapo baadhi ya watu katika jamii ambao hukosa kabisa chakula na kushinda

kama sio kulala wakiwa na njaa. Watu wa aina hii huweza kufikia uamuzi wa kufanya jambo lolote lile baya ili waweze kufanikiwa kupata chakula. Wanasosholojia wanapendekeza kuwa ni vema serikali ikawa na sera nzuri za kupambana na umasikini na kisha wakafanya kila jitihada kutekeleza sera hizo ili kuepusha mambo mabaya ambayo yanaweza kufanywa na watu wenye njaa (Held na Thomson, 2009).

Mhusika Bahati ni mfano mzuri wa mtu ambaye alitamani kupata chakula kizuri cha chaguo lake kila siku lakini hali haikuwa hivyo. Mwandishi anasema:

> Bahati kwa mara ya mwanzo katika maisha yake aliuhisi umaskini. Sasa alijua kuwa yumo katika *hali* mbaya ya umaskini; ndiye yeye mpigana na tumbo, mmezea mate (uk. 28).

Kifungu hiki cha maneno kinaonesha namna chakula kilivyo kitu muhimu katika maisha ya mwanadamu kiasi cha kumfanya mwanadamu kufanya kila analoweza ili apate chakula. Umaskini wa kukosa chakula ni mbaya kuliko umaskini wa aina nyingine. Ikiwa mtu ameshiba na anaridhika na chakula anachokula ni rahisi kwa mtu huyo kuwa na fikra pana za kujiletea maendeleo. Lakini ikiwa mtu huyo kazi yake ni kufikiria kuwa atakula nini kila mara akili yake haiwezi kufanya kazi vizuri na hivyo kuundeleza hali ya umasikini. Si hivyo tu, bali pia, mtu anapokosa chakula hawezi kuwa na afya nzuri na hivyo kukosa nguvu za kutosha kufanya kazi (Tonkiss, 2006).

### 4.2.5 Dhamira ya Ujasiriamali

Ujasiriamali ni neno linalotokana na maneno mawili ambayo ni “jasiri,” na “mali.” Maneno haya yameunganishwa pamoja na kupata neno “ujasiriamali,” likiwa na

maana kuwa ni kitendo cha mtu kuwekeza fedha au kitu chenye thamani ili aweze kupata faida zaidi kutokana na uwekezaji alioufanya. Mtu anayefanya kitendo cha ujasiariamali anajulikana kama mjasiriamali (Tonkiss, 2006). Huyu ni mtu ambaye haogopi kuwekeza kwa dhana kwamba hata pata faida na hivyo fedha au mali aliyowekeza itapotea. Mjasiriamali huamini kuwa uwekezaji atakaoufanya utamletea tija na kwamba na hata ikitokea haukuleta tija aliyotarajia atajitahidi kupambana ili kuufanya uwekezaji wake uwe imara na wenye tija. Huyu ni mtu jasiri kwani si kila mtu na si jambo jepesi mtu kuamua kufanya uwekezaji bila ya kuwa na hofu juu ya mustakabali wa uwekezaji wake huo ambao ni mpya (Anivery, 1970).

Kwa hakika ujasiriamali ni dhana ambayo imekuwepo tangu enzi na enzi lakini imepata mashiko zaidi katika miaka ya mwishoni mwa 1990 mara baada ya kuanzishwa na kuruhusiwa kwa soko huria. Ujasiriamali ulionekana kuwa ni moja kati ya maeneo ambalo linaweza kutoa ajira kwa watu wengi wakiwemo wanaume na wanawake. Kweli, kutokana na serikali kutokuwa na uwezo wa kuajiri watu wengi kwa wakati mmoja, ujasiriamali ndio unaweza kutoa ajira mpya kwa wingi zaidi. Moja kati ya makundi ya wanajamii linalojishughulisha sana na shughuli za ujasiriamali ni wanawake (Koda, 2000). Dhana ya kwamba mwanamke anatakiwa kukaa nyumbani na kusubiri aletewe kila kitu na mumewe imekwisha na haina nafasi tena katika jami. Mwanamke anatakiwa kufanya kazi za kijasiriamali ili apate kipato cha kusaidiana na mumewe katika kumudu gharama za maisha. Mohamed Suleiman katika riwaya yake ya *Kiu* anasawiri hali hii pale anaposema:

> Cheusi alizibeba kazi zote za nyumba. Usiku akisukuma maandazi na mikate ya biashara; huanzia mapema wakati wenye kelele huko nje kwa majirani zake *wakizungumza* hata kelele zikapungua, hadi

> katika shwari ya usiku wa manane asipofikwa masikioni na sauti isipokuwa ya kifimbo chake cha kusukumia maandazi na mikoromo ya majirani waliolala. Wakati huo bahati huwa kalala baada ya kusoma na kibatari chake kwisha mafuta (uk. 29).

Kifungu cha maneno kilichopo hapo juu kinathibitisha kuwa ni kweli wanawake hujishughulisha katika shughuli ndogondogo za ujasiriamali. Cheusi ni mama yake bahati ambaye alifiwa na mume na kuachiwa majukumu yote ya kumlea mtoto wao Bahati pamoja na kujilea yeye binafsi. Hakuwa na namna nyingine ya kuweza kumudu gharama za maisha bali ni kuchoma maandazi na mikate kwa ajili ya biashara. Shughuli hiyo ya kuchoma maandazi na mikate aliifanya usiku wa manane ambapo alistahili kuwa amelala kama ilivyokuwa kwa majirani zake lakini haikuwezekana kuwa hivyo. Dhana ya ujasiriamali inajitokeza katika kifungu hicho cha maneno hapo juu kwamba, mjasiriamali ni mpambanaji asiyekata tamaa na hufanya kazi hata katika mazingira magumu. Mpambanaji wa aina kama ya Cheusi hufanikiwa hata kama si kwa asilimia nyingi lakini huweza kumudu sehemu ya gharama za kuendeshea maisha yake. Kutokana na biashara ya kuchoma maandazi na mikate Cheusi aliweza kumpatia mtoto wake mahitaji ya shule pamoja na chakula ingawa ilikuwa ni aina moja tu ya chakula kama tulivyoona mahali fulani hapo juu katika tasinifu hii.

Wanasosholojia wanaeleza kuwa wanawake wana nafasi kubwa ya kufanikiwa katika shughuli za ujasiriamali kwa sababu wengi wao si wafujaji wa fedha (Held na MacGrew, 2007). Mwanamke anapopatiwa mkopo kama sehemu ya kukuza mtaji wake mara nyingi hutumia mkopo huo kama alivyoelekezwa na wakopeshaji tofauti na baadhi ya wanaume. Hivyo, mwanamke kama Cheusi anaonekana kuwa anafanya

biashara ya kuuza maandazi na mikate kwa sababu mtaji wake ni mdogo lakini akipata mtaji wa kutosha ataikuza biashara yake zaidi. Ni vyema taasisi zinazohusika na uwezeshaji wa wajasiriamali wagodo zikajitahidi kuwapatia wajasiriamali hao mitaji yenye masharti na riba nafuu ili waweze kukuza biashara zao na kuongeza kipato (Ulomi, 2003).

Katika sehemu hii tumefanikiwa kuwasilisha, kuchambua na kujadili data zinazohusu lengo mahususi la kwanza la utafiti huu. Sehemu inayofuata inawasilisha na kuchambua data zinazohusiana na lengo mahususi la pili. Lengo mahususi la pili linahusu kuchambua dhamira katika riwaya ya *Kiu* iliyotungwa na mwandhishi Mohamed Suleiman.

### 4.3 Mbinu za Kifani katika Riwaya ya Kiu

Fani ni ufundi wa kisanaa unaotumiwa na mwandishi anapoandika au kusimulia kazi yake ya fasihi mbele ya hadhira aliyoiteua kwa ajili ya kazi hiyo. Fani hujumuisha vipengele vya matumizi ya lugha, muundo, mtindo, wahusika na mandhari. Vipengele hivi kwa umoja wake ndivyo vinavyomwezesha mwandishi wa kazi ya fasihi kujenga dhamira na mawazo yake na kuyawasilisha kwa hadhira iliyolengwa. Matumizi ya vipengele vya fani hutofautiana na wakati mwingine hata kufanana baina ya mwandishi mmoja na mwingine. Mohamed Suleiman katika riwaya ya *Kiu* ametumia mbinu mbalimbali za kifani ili kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa lakini katika utafiti huu hatuwezi kushughulikia mbinu zote. Baadhi ya mbinu za kisanaa tulizozitafiti katika tasinifu hii ni mbinu ya matumizi ya barua, taharuki, misemo, sitiari na tashihisi.

### 4.3.1 Matumizi ya Mbinu ya Barua

Barua ni njia kongwe ya mawasiliano baina ya mtu na mtu, mtu na watu, taasisi na mtu, taasisi na taasisi inayolenga kutoa taarifa au ujumbe fulani ambao ni muhimu kufahamika kwa upande uliolengwa na barua hiyo (Abdalla, 2014). Barua huandikwa katika karatasi na kutiwa katika bahasha na kisha kutumwa kwa aliyelengwa kupokea barua hiyo. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia hivi sasa barua huandikwa kama ujumbe katika simu na kisha kutumwa kwa mlengwa na kumfikia mara moja. Hii haimanishi kuwa mfumo za zamani wa kuandika na kutumiana barua haupo ila inakidhi kusema kuwa umepungua kasi kutokana na maijilio ya sayansi na teknolojia na kuonekana kuwa barua za kuandika katika karatasi na kutumwa kwa mlengwa hutumia muda mrefu kumfikia mhusika (Khamis, 2007). Utumaji wa barua kwa njia ya simu na mtandao kama barua pepe unafanya barua kutumia muda wa kufumba na kufumbua macho kumfikia mlengwa.

Yote kwa yote lakini ni ukweli kuwa bado matumizi ya barua kama chombo cha mawasiliano katika jamii. Watunzi wa kazi za fasihi kama Mohamed Suleiman anatumia mbinu ya barua katika kujenga dhamira wa hadhira yake kama ifuatavyo:

> Iddi alipokea barua kwa mshangao maana hakuwa akiitazamia. Aliigeuza upande wa pili, akaona jina la *Bahati* limeandikwa kwa mkono uliokuwa wa haraka. Akaifungua na kusoma:
> Iddi,
>
> Usistaajabu nikikuambia ya kuwa hivi sasa niko kitandani kwa bwana Mwinyi, tunapanga siku ya arusi yetu ya kikweli. Si ruhusa kutuingilia kwani tuna hiari yetu. Nakuonya kwa salama yako mwenyewe, kuwa mipango yako iwe imekoma baada ya kuipata barua hii.
> Nisalimie fulani …
>
> Wa nafsi yangu,

> *Bahati*.
> Barua ile iliwasha moto moyoni mwa Iddi na kumchemsha kwa hasira. Ilimwia kama dhoruba kali ya ghafla. Mara macho yake yaligeuka rangi, kipaji kikapetana, na kidevu kikamwanguka, kwa ajabu ya uchungu. Aliisoma tena ile barua, na kila alipozidi kuisoma ndivyo alivyozidi kuchafuka kwa hasira (uk. 58-59).

Barua hii iliandikwa na bahati kwenda kwa Iddi ambaye ni mpenzi wake ambaye anampenda sana lakini hapa anamtaarifu kuwa sasa yeye amekwishakuwa na mapenzi na mtu mwingine aitwaye Mwinyi. Mwinyi ni bosi wa Iddi na Iddi alimtaka Bahati kumrubuni Mwinyi kuwa anampenda ili wapate fedha lakini anayependwa kwa dhati ni Iddi. Sasa ni jambo la kushtusha sana kuona mapenzi ya Mwinyi na Bahati yanakuwa ni ya kweli na si mzaha kama Iddi alivyotaraji. Iddi sasa anaingiwa na mashaka makubwa kama kweli utajiri alioutaka kutoka kwa Mwinyi kupitia kwa Bahati ataupata au ndio umeshapotea. Dhamira ya mapenzi na ile ya wizi na magendo zinakuzwa kwa kiasi kikubwa kutokana na matumizi ya barua iliyopo hapo juu. Bahati anapima kama kweli Iddi anampenda kwa dhati naye Iddi anapata hasira kuwa mradi wake wa kutaka kupata utajiri wa Mwinyi kupitia kwa bahati unapotea.

Pia, kupitia barua iliyopo hapo juu mwandishi anajenga dhamira kuwa si kila jambo linaweza kuwa kama vile mtu alivyotaraji liwe. Mipango na utekelezaji wa jambo ni vitu viwili tofauti ingawa vinategemeana (Scott, 1995). Iddi hakutegemea kuwa kumwambia Bahati ajidai kuwa anampenda Mwinyi ili wapate utajiri kunaweza kumfanya Bahati akampenda Mwinyi Kikweli kweli na kumuacha yeye. Hapa panajengwa dhamira ya maonyo kwamba mapenzi huwa hayajaribishwi kwani wakati na saa yoyote yanaweza kubadilika na kuwa tofauti kabisa na ilivyokusudiwa.

### 4.3.2 Matumizi ya Misemo katika Kiu

Misemo ni kauli zinazokaribiana na kushahabiana na methali itumiwayo na wanadamu kama chombo cha mawasiliano (Msokile, 1992). Hata hivyo, mara nyingi misemo huwa haina pande mbili kama ilivyo kwa methali. Methali kwa upande wake huwa na pande mbili ambapo upende mmoja huwa ni kama swali na upande wa pili huwa ndio jibu la swali lililoulizwa (Wamitila, 2003). Misemo ni kauli ambazo hutokana na misimu ambayo kanuni yake ni kuwa huibuka na kupotea na ile ambayo haipotei inadumu ndio huitwa misemo. Misemo ni mbinu ya kifani inayotumiwa na watunzi wa kazi za fasihi ili kukazia au kutoa msisitizo juu ya dhamira fulani ambayo wanataka hadhira yao ipate. Mohamed Suleimani katika riwaya yake ya Kiu ametumia misemo katika kazi yake hii kama ifuatavyo:

> Watu waliposema kuwa hakuna aliyepata kumwia Mwinyi, maneno yao hayakuwa yametiwa *chumvi*. Mwinyi alikuwa na fedha za kutosha kujinunulia vingi ya vile mzee wa miaka sitini na miwili kama yeye angevitamani isipokuwa kitu kimoja tu. Hicho ndicho kilichomfanya hata akaona kama kwamba umri wake wote alioishi umepotea bure, na ule **utajiri wake mfano wa kitumbua kilichotiwa mchanga** (uk.01).

Maneno yaliyokolezwa wino katika kifungu cha maneno hapo huu ni msemo unaoashira kuwa jambo au kitu kizuri sasa kimekuwa kibaya, kitu kitamu sasa kimekuwa kichungu na kitu cha thamani sasa thamani yake imepotea. Mzee Mwinyi alikuwa ni tajiri mwenye kila aina ya mali lakini alitamani kuwa na mapenzi na binti aliyetokea kumpenda sana akiitwa Bahati. Kila mbinu aliyoitumia haikufanikiwa katika kumfanya Mwinyi ampate Bahati ndipo hata akalalamika kuwa, “utajiri wake mfano wa kitumbua kilichotiwa mchanga,” kwamba utajiri wake haumsaidii na wala hauna faida yoyote ile kwake. Kimsingi, kitumbua ambacho kinakuwa kimetiwa

mchanga huwa hakiliki na ladha yake yote hupotea kwa sababu mlaji huogopa meno yake kutafuna mchanga. Msemo huu kwa hakika umetumika katika kutoa msisitizo wa dhamira ya mapenzi kuwa ikiwa mtu ni tajiri wa kila kitu lakini anapokosa mapenzi aliyoyatamani basi utajiri wake huwa si lolote na humfanya aishi kwa taabu na adha ya mawazo kiliko hata mtu maskini. Wanasosholojia wanakiri kwamba vipo baadhi ya vitu ambavyo huonekana ni bora sana mtu kuwa navyo mathalani utajiri (Cross, 2011). Lakini hufika mahali mtu akakosa kitu ambacho alidhani kuwa ni kidogo na ule utajiri wake usimsaidie katika kukipata kitu hicho hali yeye aliamini kuwa utajiri wake ndio silaha ya kupata kila kitu. Hii ni sawa na kusema kuwa, sasa kitumbua kimeingia mchanga kwani utajiri wote wa Mwinyi haukumwezesha kupata mapenzi ya Bahati.

Matumizi mengine ya msemo yanajitokeza pale ambapo Cheusi ambaye ni mama yake Bahati alipokuwa akimuonya mwanawe juu ya mahusiano yake na Iddi. Anasema:

> Palikuwa na kimya kifupi lakini kichungu. Halafu Cheusi akazidi kumshauri: "Huyo Iddi wako huyo, nikwambie, hana kukutaka, hana chochote. Anayemta*ka mwanamke* humuoa. Yeye anataka akuchezee na halafu akutupilie mbali, apite akikucheka. Nimekwishatambua kama wewe umesoma hicho Kizungu chako unaniona mimi mjinga basi haya … **Utakuja lia kilio cha mbwa mdomo juu**, mimi niko hapa (uk. 25-26)."

Katika kifungu hiki cha maneno mwandishi anatumia msemo, "utakuja lia kilio cha mbwa mdomo juu," kurejelea dhamira ya malezi na maonyo yanayotolewa na mama kwa mwanaye. Cheusi alikuwa akimuonya mwanaye Bahati kuwa mahusiano yake aliyoanzisha na Iddi hayakuwa mazuri kwake kwani lengo la Iddi halikuwa ni la

kumpenda kwa dhati bali kumchezea tu. Wazazi waliuo wengi wanafahamu kuwa, vijana wanapokuwa na mahusiano ya kimapenzi kabla ndoa mara nyingi huishia kuchezeana na suala la kuoana hupotea. Hivyo, kama mzazi Cheusi alimtaka binti yake aachane mara moja na Iddi. Msemo uliotumika katika kifungu hapo juu umetumika kujenga na kutoa msisitizo wa dhamira ya malezi ya mama kwa mto wake. Wanasosholojia wanaeleza kuwa mazoe ni kitu kinachojenga tabia na daima mazoea huendelea daima (Ritzer, 2008). Kama katika jamii wasichana na wavulana wanaachwa huru kuwa na mahusiano kabla ya ndoa watalifanya hilo kuwa ni jambo sahihi na suala la kufunga ndoa halitakuwa na umuhimu kwao tena. Ni lazima wazazi wafanye kazi yao vizuri ili wanajamii hasa vijana waone kwamba kuwa na mahusiano kabla ya ndoa ni kitu kibaya na hakifai kuenziwa hata mara moja.

### 4.3.3 Matumizi ya Sitiari katika Kiu

Sitiari ni tamathali ya usemi inayotumika katika kulinganisha vitu viwili vyenye sifa tofauti bila ya kutumia kiunganishi vya kufananisha kama ilivyo katika tashibiha (Kyando, 2013). Vitu vinavyolinganishwa huchukuliwa kuwa ni sawa sawa kabisa na havina tofauti yoyote ile. Kwa mfano, mtu anaweza akasema "Mwajuma ni sungura mdogo aliyejificha juu ya mti." Hapa Mwajuma anafananishwa na sungura kana kwamba ni vitu viwili vilivyo sawa sawa bila ya tofauti hata kidogo. Lengo hasa la kutumia sitiari katika kazi za fasihi ni kutoa msisitizo juu ya dhamira inayowasilishwa kwa msomaji. Mohamed Suleiman ametumia sitiari pale aliposema:

> Pende hivi, Iddi, dereva wake aliingia bila ya kubisha hodi. Mwinyi alishtuka na kumuuliza, "mbona *umekawia*?"
> Iddi alifuta jasho kuonesha jitihadi aliyofanya, akatikisa kichwa kwa masikitiko na kusema, "nimekuta kufuli *mlangoni*."

> **Maneno yale yalimkata Mwinyi ini lake**. Alishusha mabega akanywea juu ya kiti, akaona maisha yakimwonea. Kusubiri kusiko kikomo-miezi sita imepita na kutamani kusiko danganyika kukimtwesha. Alikuwa amekwishavumilia vya kutosha; bado hakujua ni lini siku ya faraja. Lakini ah, maneno ya marehemu mama yake: Likufikalo patana nalo (uk.02).

Matumizi ya sitiari katika kifungu cha maneno hapo juu yanabainisha kuwa maneno yamefafanishwa na kisu au kitu chochote ambacho ni kikali chenye uwezo wa kukata kitu. "Maneno yale yalimkata Mwinyi ini lake," ni kauli yenye kuonesha kuwa matumaini ya Mwinyi kumpata Bahati yalikwishapotea mara baada ya taarifa kutoka kwa Iddi kuwa amemkosa Bahati na mlango wa nyumba ya Bahati umefungwa.

Wanasosholojia wanaeleza kuwa mwanadamu hufika mahali akakata tamaa juu ya kupata kitu fulani ambacho alitaraji kukipata kwa muda mrefu na asikipate (Webster, 2006). Kukata tamaa katika maisha ni jambo baya kwani huweza kumfanya mtu akafanya jambo baya ambalo hata linaweza kudhuru watu wengine. Kwa mfano, kitendo cha Mwinyi kukata tamaa ya kumpata Bahati kinaweza kikamfanya Mwinyi kuja na maamuzi ya kufanya uhalifu wa kubaka. Kitendo cha ubakaji ni kibaya kwa ambaye atakuwa amebakwa lakini pia kwa mbakaji kwani huweza kuishia jela katika maisha yake yote yaliyobakia. Mzee wa miaka sitini na miwili kama Mwinyi kufungwa jela ni kitu kibaya ambacho kinaweza kumfanya akafia huko jela.

### 4.3.4 Matumizi ya Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ya usemi inayotumika katika kuvipa urari na uwezo wa kutenda kama binadamu viumbe au vitu ambavyo havina uwezo huo (Mlacha, 1989). Vitu kama vile miti, maneno, wadudu, wanyama na ndege wanaosawiriwa wakifanya

vitendo vya kibinadamu hali ya kuwa hawana uwezo wa kufanya vitendo hivyo. Kwa mfano, si jambo la ajabu kuona katika fasihi ndege wakichumbiana na kupeleka posa la kuoa na hatimaye ndoa hufungwa na ndege hao wakaishi raha mustarehe (Senkoro, 2006). Matumizi ya tashihisi katika kazi za fasihi hufanywa kwa lengo la kujenga dhamira kitaswira ili kumfanya msomaji atafakari kidogo ndipo aweze kupata dhamira iliyokusudiwa na mwandishi au msimuliaji wa kazi iliyo mbele yake. Katika riwaya ya Kiu kuna matumizi ya tashihisi yaliyotumiwa kwa lengo kama hilo ambayo yanajitokeza kama ifuatavyo:

> Bahati alilia kwa kite na *simanzi*, **hata usingizi ukamuonea huruma, ukamchukua hima na kumpumzisha kitandani**. Alizindushwa na vishindo vya *waenda* msikitini, maana tayari kulikwisha pambazuka. Saa ya Bahati, siku zote ilikuwa wapiti njia. Alikuwa amekwishazoea kusikia wakati wa nyendo za wale waendao kazini, shule, misikitini, ndege za abiria, na waadhini (uk.20).

Maneno yaliyokolezwa wino katika kifungu cha maneno hapo juu yametumiwa kitashihisi kwani katika maisha halisi ni mwanadamu pekee ndiye mwenye urari wa kuwa na huruma kwa mtu au kiumbe mwingine yoyote. Usingizi ni hali ya mtu kulala akawa hana fahamu kwani Waswahili husema, “usingizi ni nusu ya kufa.” Hata hivyo, katika kifungu cha maneno hapo juu inaonekana kuwa usingizi umepewa uwezo wa kuwa na huruma kama mwanadamu.

### 4.3.5 Matumizi ya Taharuki katika Kiu

Taharuki ni mbinu ya kifani inayotumiwa na watunzi wa kazi za fasihi katika kuzisana kazi zao hata zikafikisha dhamira zilizokusudiwa kwa hadhira iliyolengwa. Hii ni mbinu ya kumcheleweshaa msomaji katika kupata suluhisho au ukweli wa mambo ulivyo na kumfanya aendelee kusoma zaidi mpaka pale atakapokutana na

suluhisho au maelezo fulani yatakayompatia jawabu alilokusudia kulipata (Senkoro, 2006). Mbinu ya taharuki hutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi kwa makusudi mazima ya kumpatia msomaji au msikilizaji hamu ya kusoma hasa kazi husika inapokuwa ni ndefu kiasi cha kumchosha msomaji. Urefu wa kazi utaonekana kuwa ni mfupi sana kama kutakuwa na taharuki zenye kumvutia msomaji. Taharuki ni mbinu kongwe ya kifani inayotumika sana katika fasihi simulizi na hata katika fasihi andishi. Mohamed Suleiman katika riwaya yake ya Kiu ametumia mbinu hii kwa namna alivyoanza kusimulia hadithi yake. Kwa mfano:

> Jioni hiyo alikuwa amejinyoosha juu ya kiti cha kulala, macho yake kayatupa darini, akihesabu dakika. Tamaa yake haikuwa kubwa, na wasiwasi wa kutofaulu ulimwondolea furaha. Lau kuwa alichokitaka kilikuwamo mikononi mwake, angekigugumia na kukata kiu yake. Lau kuwa alichokitaka kingenunulika kwa fedha, bila shaka angezikwangua zote alizonazo. Lakini kitu chenyewe kilikuwa ni hiari ya mtu mwingine, mwenye tadi na kiburi. Kwa hivi alikuwa hana budi kuomba na kusubiri (uk.01-02).

Kifungu hiki cha maneno kina taharuki ndani yake ambapo kuna jambo linalomfanya Mwinyi kutokuwa na raha na kumtesa licha ya kuwa yeye ni tajiri. Kitu hicho hakisemwi bayana bali inasemwa tu kama kupatikana kwa kitu hicho kulihitaji fedha basi Mwinyi angetoa fedha zote za utajiri wake. Hata hivyo inaelezwa kuwa kitu chenyewe kilikuwa ni hari ya mtu tena mtu huyo ana kiburi na maringo. Maelezo haya yanaonyesha kuwa kitu hicho hakikutajwa kuwa ni kitu gani jambo ambalo linamfanya msomaji aliye makini kutaka kujua kulikoni hata jambo hilo likamshughulisha Mwinyi kiasi hicho?

Matumizi hayo ya taharuki yatamfanya msomaji aendelee kusoma riwaya ya Kiu mpaka pale atakapolifahamu hilo jambo ambalo linamsumbua Mwinyi. Kadri

anavyoendelea kusoma ndipo anapokutana na maneno haya:

> "Ati watu *husema* mapenzi hayakutani, mbona yako wewe na Bahati yamekutana?"
>
> "Wacha masihara Iddi," *Mwinyi* alimkaripia. "Unafikiri mtoto kama yule anaweza *kumpenda* mzee kama mimi (uk.05)?"

Katika kifungu hiki taharuki iliyojengwa na mwandishi katika ukurasa wa kwanza wa riwaya yake inaanza kupata majawabu katika ukurasa wa tano. Hapo ndipo linapotajwa jambo linalomshughulisha Mwinyi kiasi cha kukosa raha pamoja na utajiri wake mkubwa alionao. Kitu hicho si kingine bali ni mapenzi aliyokuwa nayo kwa binti aliyejulikana kwa jina la Bahati. Mwinyi alikuwa ni Mzee wa miaka sitini na miwili lakini alimpenda sana Bahati ambaye ni binti mdogo hata shule bado hajamaliza. Katika mazingira haya panajengeka tena taharuki nyingine ya kwamba Bahati anaweza kukubali kuwa mpenzi wa Mzee mtu mzima kama alivyo Mwinyi? Hii nayo ni taharuki kwa wasomaji ambapo watavutiwa kusoma zaidi ili waweze kuona ni nini kitatokea juu ya mapenzi ya Mwinyi kwa binti Bahati.

Matumizi ya mbinu hii ya taharuki yametumiwa kwa lengo la kukuza na kuendeleza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kiu*. Mbinu hii inaonekana kutumiwa kwa mfululizo kwani pale jawabu au suluhisho la taharuki ya kwanza linapopatikana basi taharuki nyingine huibuliwa (Mlacha, 1991). Mathalani, katika kifungu cha maneno hapo juu tumepata suluhu kuwa jambo lilokuwa likimsumbua Mwinyi raha na kumkosesha usingizi ni mapenzi yake kwa binti Bahati. Baada ya kulijua hilo, imejengwa taharuki nyingine ya kuwa hivi binti mdogo kama Bahati anaweza kuridhia kuwa na mapenzi na Mzee Mwinyi ambaye anaweza kumtukuu Bahati?

Wasomaji wataendelea kusoma zaidi mpaka pale watakapopata suluhisho na baada ya hapo watapata taharuki nyingine.

### 4.4 Hitimisho

Hii ndiyo sura iliyoshughulikia uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti na kufanikisha kukamilika kwa utafiti huu. Uchambuzi wa data za utafiti ulifanywa kwa kurejelea malengo mahususi ya utafiti ambapo katika utafiti huu kulikuwa na malengo mahususi mawili. Malengo hayo yalikuwa ni kuchambua dhamira za kijamii katika riwaya ya *Kiu* iliyoandikwa na Mohamed Suleiman na kuelezea mbinu za kifani zilizotumika katika kujenga dhamira za kijamii katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman. Hivyo, yaliyojiri katika sura hii kwa mujibu wa lengo mahususi la kwanza ni dhamira ya usafi wa mazingira, mapenzi katika jamii, wizi na magendo, umaskini katika jamii na ujasiriamali. Kwa upande wa lengo mahususi la pili yaliyojiri ni pamoja na matumizi ya mbinu za kifani za barua, misemo, sitiari, tashihisi na taharuki.

# SURA YA TANO

# 5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa hitimisho, muhtasari na mapendekezo kuhusu utafiti mzima pamoja na matokeo yake. Sura hii inafupisha mambo mengi yaliyosemwa katika utafiti huu ili kumwesha msoamji kupata picha ya utafiti mzima pale anaposoma sura hii.

## 5.2 Muhtasari

Kwa kuwa data za utafiti ziliwasilishwa, kuchambuliwa na kujadiliwa kwa mujibu wa malengo mahususi na muhtasari wa sura hii pia umetolewa kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti.

### 5.1.1 Dhamira za Kijamii katika Riwaya ya Kiu

Dhamira za kijamii kama tulieleza hapo awali kuwa hizi ni dhamira ambazo zinahusu maisha ya kila siku ya wanadamu. Ni dhamira ambazo zinatokana na shughuli mbalimbali za jamii katika harakati za kudumisha maisha yao. Katika riwaya ya Kiu kuna utajiri mkubwa wa dhamira za kijamii lakini katika utafiti huu ni 5 tu ndizo zilizowasilishwa, kuchambuliwa na kufanyiwa mjadala. Dhamira hizo ni usafi wa mazingira, mapenzi katika jamii, wizi na magendo, umaskini katika jamii na ujasiriamali. Tukieleza kwa muhtasari kuhusu dhamira ya usafi wa mazingira kama ilivyosawiriwa katika riwaya ya *Kiu* mwandishi anabainisha kuwa jamii usafi wa mazingira bado ni changamoto kubwa katika jamii. Jamii hafanyi jitihada kubwa katika usafi wa mazingira licha ya kuwa wao ndio watumiaji wa mazingira na ndio

wanaosababisha uchafuzi wa mazingira. Pia, serikali nayo bado haikufanya jitihada kubwa katika usafi wa mazingira jambo linalosababisha miji kuwa michafu na kuibuka kwa magonjwa ya kuambukiza kama kipindupindu na homa za matumbo.

Dhamira nyingine ambayo tunaweza kuieleza kwa muhtasari ni ile ya wizi na magendo ambayo imesawiriwa vizuri katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman. Mtunzi anathibitisha kuwa wizi na magendo ni vitu ambavyo kwa sasa vimetawala katika jamii kwani watu wengi hupata utajiri wa mali kutokana na njia za wizi na magendo. Tabia hii imezoeleka katika jamii kiasi cha kufanya wanajamii kuamini kuwa wanaweza kupata utajiri kwa njia za wizi na magendo na utajiri wao ukawa ni wa uhalali. Kashifa za rushwa na ufisadi zimekuwa nyingi katika jamii ya Watanzania kiasi cha kufanya kila idara na taasisi za serikali na za binafsi kuhusishwa na rushwa. Jambo hili si jema hata kidogo na linapaswa kukomeshwa ili likome kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi ya Tanzania.

Ujasiriamali ni dhamira nyingine ambayo imejitokeza kwa kiasi kikubwa katika riwaya ya Kiu. Kama tulivyosema mahali fulani katika tasinifu hii ni kuwa katika jamii ya leo kila kitu kimekuwa ni bidhaa kiasi kwamba kama mtu hana fedha hawezi kuishi maisha mazuri. Ujishughulishaji wa akina mama hasa kwa kuanzisha biashara ndogo ndogo za kijasiriamali kumesaidia kuwawezesha akina mama kumudu gharama za maisha hata pale wanapofiwa na waume zao. Mfano mzuri ni Cheusi ambaye alifiwa na mumewe na kisha kuachwa na mtoto ambaye alikuwa ni mwanafunzi. Kwa kufanya shughuli ya kusukuma maandazi na mikate aliweza kupata fedha ambazo zilimsaidia kuendesha maisha yake na mtoto wake ingawa

fedha hizo hazikuwa za kutosheleza. Huu ni mfano mzuri ambao unafaa kuigwa na akina mama wengine kwa kuwa ni kitu ambacho kinawezekana.

Dhamira nyingine zilizowasilishwa, kuchambuliwa na kujadiliwa ni pamoja mapenzi katika jamii na umaskini. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa ipo dhana kuwa mwanamke maskini anaweza kumkubali mwanaume yeyote tu alimradi anao uwezo wa kifedha. Dhana hii alikuwa nayo Iddi ambaye ni dereva wa Mzee Mwinyi kwa miaka mingi. Iddi aliamini kuwa Mwinyi anaweza kumpata Bahati kwa sababu yeye alikuwa ni tajiri na Bahati alitoka katika familia ya kimaskini. Mawazo haya yanaweza kuwa na ukweli fulani lakini pia yasiwe na ukweli katika baadhi ya mazingira. Hata hivyo, mapenzi yanayosabishwa na watu kupenda fedha ni mengi zaidi kuliko yale ya mtu kumkataa mtu kutokana na utajiri wake.

### 5.1.2 Mbinu za Kifani katika Riwaya ya Kiu

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa Riwaya ya Kiu ya Mohamed Suleiman inasheheni utajiri mkubwa wa mbinu za kifani lakini katika utafiti huu tumeshughulikia vipengele vya matumizi ya mbinu ya barua, misemo, sitiari, tashihisi na taharuki tu. Sababu hasa ya kuteua mbinu hizi 5 ni kuwa zinatosheleza mahitaji ya malengo ya utafiti huu. Mbinu ya matumizi ya barua imetumiwa kwa lengo la kukuza na kuendeleza dhamira ya mapenzi ambapo Bahati alitaka kujua kama Iddi anampenda kwa dhati. Bahati aliandika barua ya kumweleza Iddi kuwa sasa yeye bahati yupo katika mapenzi ya dhati na Mwinyi na anamuomba Iddi asimsumbue kwani hivi sasa wapo katika mipango ya harusi yao. Barua hiyo ilimtesa Iddi hata asijuwe ni jambo gani atafanya kwa sababu tayari alikwishafahamu

kwamba mipango yote aliyoipanga yeye na Bahati sasa imekufa. Hata hivyo, yaliyosemwa katika barua hiyo yalilenga kumpima Iddi kama kweli anampenda Bahati. Bahati alifahamu kuwa Iddi anampenda kwa sababu alikasirika baada ya kuisoma barua aliyomtumia. Kumbe Iddi hakukasirika kwa sababu alimpenda sana Bahati bali aliona dhahiri kuwa mipango ya kupata utajiri wa Mwinyi kupitia kwa Bahati ilikuwa ni ndoto tu isiyotekelezeka tena.

Taharuki ni mbinu nyingine ya kifani ambayo imetumika katika kuibua dhamira za kijamii katika riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman. Mbinu hii imetumika katika upangaji wa visa na matukio ambapo mwanzo tu wa riwaya hii pameanza kitaharuki. Hali ya kumchelewesha msomaji kupata suluhisho la kile ambacho kinaelezwa katika riwaya kinamfanya msoamji kuwa na hamu ya kusoma zaidi kwani atataka kusoma zaidi ili apate mwisho wa tukio lake. Kwa mfano, mwanzoni mwa riwaya kunaelezwa kuwa Mwinyi anaishi kwa shida na kukosa raha licha ya kuwa yeye ni mtu tajiri. Jambo linaloezwa kuwa ndilo linalomnyima Mwinyi raha ni mapenzi yake kwa Bahati jambo ambalo aliona kuwa haliwezi kufanikiwa kutokana na yeye kuwa na ni Mzee na Bahati ni binti mdogo.

Mbinu nyingine za kifani zilizotumika katika kujenga dhamira za kijamii katika riwaya ya Kiu ni misemo, sitiari na tashihisi. Mbinu hizi za kifani zimetumika katika kusisitiza masuala mbalimbali yanayohusiana na dhamira za kijamii katika riwaya ya *Kiu*.

## 5.3 Hitimisho

Riwaya ya *Kiu* licha ya kuandikwa zaidi ya miaka 44 iliyopita lakini bado dhamira zinazoelezwa katika riwaya hii ni zimejaa uhalisia wa mambo ulivyo katika jamii ya leo ya Watanzania. Dhamira za usafi wa mazingira, mapenzi, wizi na magendo, umaskini na ujasiriamali ni dhamira zilizopamba moto katika Tanzania ya leo. Kwa mfano, kuhusu usafi wa mazingira, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania daktari John Pombe Joseph Magufuli alifuta sherehe za uhuru za tarehe 9 mwezi wa 12 mwaka 2015 na kuifanya siku hiyo kuwa ni siku ya usafi wa mazingira nchi nzima. Aliamua kuchukua uamuzi huo kwa sababu nchi ilikuwa imekumbwa na ugonjwa wa kipindupindu unaosababishwa na uchafu wa mazingira.

Riwaya ya Kiu imesheheni dhamira ambazo zina uhalisia katika maisha ya leo ya jamii. Dhamira hizo ni pamoja ujasiriamali ambapo tunaona kundi la wanawake likijitokeza na kushiriki katika uzalishaji mali na kufanya biashara. Shughuli za uzalishaji mali husaidia katika kukuza kipato na kupunguza umaskini uliopo katika jamii. Dhamira hizi zimewasilishwa kupitia mbinu za matumizi ya barua, misemo, sitiari, tashihisi na taharuki.

## 5.4 Mapendekezo

Tunapendekeza utafiti kama huu ufanyike kwa kulinganisha dhamira katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Kiu* zote za Mohamed Suleiman ili kuona namna anavyosawiri dhamira za kijamii.

Pia utafiti kama huu unaweza kufanyika katika kulinganisha na kulinganua matumizi ya mbinu za kifani katika riwaya za *Nyota ya Rehema* na *Kiu* zote za Mohamed Suleiman ili kupata muktadha mzima wa mbinu za kifani katika riwaya zake.

**MAREJELEO**

Abdallah, A. O. (2014), "Kuchunguza dhamira za Kijamii na Kiutamaduni katika Riwaya za Shafi Adam Shafi: Mfano wa Kuli na Vuta N'kuvute," Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

ALli, A R. (2015), "Kuchunguza Dhana Zinazobebwa na Wahusika na jinsi Zinavyolandana na Majina yao: Uchunguzi Kifani wa Kiu na Kiu ya Haki," Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania,

Anivery, S. (1970), *The Social and Political Thought of Karl Marx*, Cambridge: Cambridge University Press.

Babie, E. (1999), *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Chachage, S. C. (2002), *Makuadi wa Soko Huria*, Dar es Salaam: E&D Company.

Creswell, J. W. (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Cross, S. (2011), *Sociological Theory and Analysis*, London: University of London.

Diegner, L. (2011), "Mazungumzo na Adam Shafi Juu ya Uandishi wake wa Riwaya," katika, *Swahili Forum* 18: 37-68.

Hawthorn, J. (1985), *Studying the Novel: An Introduction*, New Delhi: Universal Book Stall.

Held, D. & A. MacGrew, (2007), *The Global Transformation Reader*, Cambridge: Cambridge Polity Press.

Held, D. & J. B. Thomson (2009), *Sociological Theory of Mordern Society*, Cambrige: Cambridge University Press.

Kezilahabi, E. (1976), “Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya,” Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (1990), *Nagona*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1991), *Mzingile*, Dar ear es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (2003), “Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi,” katika, *Makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili namba 3*, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 226-243.

Khamis, S. A. M. (2007), “Utandawazi au Utandawizi?: Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai,” katika *Kiswahili*, Juzuu namba 70, Dar es Salaam: TUKI, Kur.47-66.

Koda, B. (2000) “The Gender Dimension of Land Rights in Tanzania: Case Study of Msindo Village, Same District”, Unpublished *Ph.D Thesis,* UDSM.

Kothari, C.R., (2008), *Reserch Methodogy: Methods and Techiniques* New Delhi: New Age Internationl Publising Ltd.

Kyando, L. (2013), “Majina Sadfa ya Wahusika katika Kusadikika na Kichwamaji,” katika *Mulika* namba, 31, TATAKI, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, kur. 37-50.

Madumullah, J.S. (2009), *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Nairobi: Sitima Printers and Stationary.

Mbise, I. (1996). *Creative Writing.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mhando, P. & Balisidya, N. (1976), *Fasihi na Sanaa za Maonesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mlacha, S. A. K. (1987) "The Portrayal of Cultural Conflict in Kiswahili Prose Fiction; A Structual Study of the Novels of Euphrase Kezilahabi" Phd. Thesis, University of London.

Mlacha, S. A. K. (1989), "The Use of Methaphor in Kezilahabi's Novel: *Rosa Mistika*," katika *Kiswahili*, Juzuu namba 56, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 25-35.

Mlacha, S. A. K. (1991), "Point of View as Stylistic Device in Kiswahili Novels," in *Kiswahili* Vol. 58, Dar es Salaam: TUKI.

Mlacha, S. A. K. na J.S. Madumulla, (1991), *Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mohamed, S. A. (2000), *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S. A. (2006), *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S. M. (1978), *Nyota ya Rehema*: Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S. M. (1985), *Kiu*, Nairobi: East African Publishing House.

Msokile, M. (1992), *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Education Publishers and Distributor, Ltd.

Mulokozi, M. M. (1996), *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (2013), "Makuadi wa Soko Huria (Chachage S. Chachage) katika Muktadha wa Riwaya ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili," katika *Mulika* Namba, 31, TATAKI, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, kur 51-66.

Njogu, K. & Chimerah, C. (1999). *Ufudishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.* Nairobi: JKF.

Nkwera, F. V. (1978), *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Nyerere, J. K. (1977), *Ujamaa: The Basis of African Socialism*, Dar es Salaam: Tanganyika Standard.

Ritzer, G. (2008), *Modern Sociological Theory*, New York: University of Maryland.

Scott, J. (1995), *Sociological Theory: Contemporary Debate*, Cheltenham: Edward Elgar.

Senkoro, F. E. M. K. (2011), *Fasihi Andishi*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Senkoro, F. E. M. K., (2006), "Fasihiya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi", katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu, 1. Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam uk. 61-68.

Skeggs, B. (1997), *Formation of Class and Gender*, London: Routledge.

Skidmore, W. (1979), *Theoretical Thinking in Sociology*, Cambridge: Cambridge University Press.

Swingewood, A.A. (2000), *A Short History of Sociological Thought*, Houndsmills: Palgrave.

Tonkiss, F. (2006), *Contemporary Economic Sociology*, London: Routledge.

Turner, B. (1999), *Classical Sociology*, London: Sage.

Ulomi, D. (2003), *Small and Medium Enterprises in Tanzania*: Dar es Salaam University Press.

Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2013), "Mikakati ya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili," katika *Mulika* namba, 32, TATAKI: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Wamitila, K. W., (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.

Webster, F. (2006), *Theories of the Information Society*: London: Routledge.

Yin, R. K. (1994), *Case Study Research: Design and Methods,* (2nd eds.) thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

Young, P.V., (1984). *Scientific Social Surves and Research*, Englewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.